# Nipashe

Alhamisi Machi 7, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579859

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US







## Tume kuundwa kuchunguza unyanyasaji kijinsia SAUT

UKURASA 3



# Katoliki watoa waraka mzito

• **Ni** ujumbe wa Kwaresma, wagusa talaka, michepuko, uchumba sugu, watoto yatima, kurithi wajane... *Ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**MAVUNDE 'APIGIA SALUTI' TOTAL KUSAIDIA VIJANA**

NAIBU Waziri wa Kazi na Vijana, Antony Mavunde, ameipongeza kampuni ya Total Tanzania...

UKURASA WA 4

**MALUMBANO YAWEKA KIPORO HATIMA DHAMANA YA MBOWE**

MALUMBANO hoja za mawakili yamesababisha hatima ya kutenguliwa uamuzi wa kuwafutia...


## Makonda awaonya waishio bondeni

UKURASA 2







UKURASA 2

Askari wa Magereza wakimsaidia Mwalimu Respicius Mtazingira, aliyehukumiwa kunyongwa hadi kufa katika Mahakama Kuu Kanda ya Bukoba jana, baada ya kupatikana na hatia ya kusababisha kifo cha mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kibeta, Spelius Eradius, mwaka jana. **PICHA: RESTUTA DAMIAN**

## Mwalimu aanguka kizimbani kwa kuhukumiwa kunyongwa


**MICHEZO** **KAGERE, BOCCO WATOA NENO JS SAOURA** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Serikali yatahadharisha wa mabondeni kuhama

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amewataka wananchi wanaoishi mabondeni kuanza kuhama kwa tahadhari ya mvua kubwa zinazotarajia kunyesha na kusababisha mafuriko.

Makonda alitoa tahadhari hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari na kuwataka wananchi kuchukua tahadhari za mvua hizo akieleza kuwa hali inaweza kuwa mbaya.

"Mkoa wa Dar es Salaam umeamua kutoa tahadhari mapema kwa sababu mvua zitakazonyesha safari hii ni kubwa na kama hatua hazitachukuliwa mapema zinaweza kuleta

INAENDELEA UK. 26



Rais Dk. John Pombe Magufuli akipakwa majivu na Paroko Msaidizi wa Parokia ya Kanisa Kuu la Mtakatifu Joseph, jijini Dar es Salaam, Joseph Mosha, wakati wa Ibada ya Jumatano ya Majivu kanisani hapo jana. **PICHA: IKULU**

# Katoliki watoa waraka mzito

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) limetoa waraka mzito likiainisha mambo 20 ambayo limesisitiza kuwa ni changamoto kwa familia kwa sasa.

Kwa mujibu wa waraka huo ambalo lenyewe limeuita Ujumbe wa Kwaresma, baraza hilo limeuteua mwaka huu kuwa ni mwaka wa familia, kama ishara na fursa ya kutafakari kwa undani zaidi matunda ya maadhimisho ya Jubilei ya miaka 150 ya kanisa hilo nchini.

Ujumbe huo wa TEC umebainisha changamoto zinazoikabili familia TEC kuwa ni pamoja na talaka, ndoa za utotoni, uchumba sugu, ndoa za mitaala, kukosa uaminifu ndani ya ndoa, ndoa za kurithi wajane na ndoa za jinsi moja.

Changamoto nyingine ni ndoa baada ya ndoa ya kwanza halali, ndoa zisizo na watoto, kubadili maumbile, familia za mzazi moja, familia zenye mchanganyiko wa imani na familia zinayoishi katika mazingira magumu ya uchumi.

Nyingine ni familia zenye watoto walemavu, familia zisizo na mzazi hata mmoja, familia zisizoishi imani, familia zisizo na maadili, familia zilizopoteza uwezo wa kulea na familia zisizo na kipato.

Katika ujumbe wake huo, TEC inabainisha kuwa asili ya matatizo katika ndoa na familia ni pamoja na utamaduni na mazingira kutokana na kuishi katika historia yenye mazoea, mila, desturi na mapokeo ya wazee.

"Iko sehemu ya utamaduni wetu isiyokubaliana na ukweli wa kimungu ambao ni wa lazima katika kuishi ndoa safi na familia bora," TEC ilinaeleza katika ujumbe wake huo.

"Mpaka sasa, katika mazingira yetu zipo tamaduni zinazoruhusu talaka, ndoa za utotoni, uchumba sugu, ndoa za mitaala, 'nyumba ndogo', ndoa za kurithi wajane, ndoa za jinsia moja na ndoa baada ya ndoa ya kwanza halali.

"Harakati hizi zinatangaza na kupigia upatu uhuru usio wa kweli kwa mwanadamu. Zinapotosha ukweli kwa kutenganisha ukweli wa maisha na ukweli wa asili katika viumbe na maumbile yao.

"Maisha ya kiroho ya ndoa na

INAENDELEA UK. 26

# Mwalimu aanguka kizimbani

**Restuta Damian,** BUKOBA

MWALIMU Respicius Mtazingira, jana alianguka kizimbani baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Bukoba kumhukumu kunyongwa hadi kufa.

Mahakama hiyo ya juu ilitoa adhabu hiyo kubwa baada ya mwalimu huyo kupatikana na hatia ya kumpiga na kusababisha kifo cha mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kibeta, Manispaa ya Bukoba, Spelius Eradius.

Vilevile, Mahakama hiyo pia imemwachia huru Mwalimu Harieth Gerald aliyekuwa mshtakiwa wa pili katika kesi hiyo ya mauaji namba 56 ya mwaka 2018.

Akisoma hukumu hiyo jana, Jaji Mfawidhi Lameck Mlacha, alisema Mahakama imejiridhisha bila kuacha shaka kuwa ushahidi uliotolewa na Upande wa Jamhuri kupitia mashahidi tisa, uliendana na kesi iliyokuwa ikiendelea.

Alisema alipata muda wa kusikiliza mashahidi wote tisa ambao wote walijiamini na hawakutetereka na kwamba mashahidi

INAENDELEA UK. 26

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
04 - 03 - 2019

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 12-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar -Es -Salaam** kuelekea **Singida**, gari hilo lenye namba za usajili:

**T 135 CCP / T 161 BDU**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

Urefu - mita 28
Upana - mita 3.7
Kimo - mita 5.4

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam hadi Singida Kupitia Morogoro,** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

xxxxxxxx

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
06 - 03 - 2019

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 14-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar -Es -Salaam** kuelekea **Kyela** , gari hilo lenye namba za usajili:

**T 275 CZS / T 321 DDH**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - mita 20**
**Upana - mita 2.84**
**Kimo - mita 4.80**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam** hadi **Kyela Kupitia Iringa,** gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

xxxxxxxx

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
06 - 03 - 2019

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 14-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar -Es -Salaam** kuelekea **Mtwara,** gari hilo lenye namba za usajili:

**T 418 DFE / T 387 DHQ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - mita 20**
**Upana - mita 2.84**
**Kimo - mita 4.80**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam hadi Mtwara Kupitia Nangurukuru,** gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

xxxxxxx

## HABARI KITAIFA

# Tume kuundwa kuchunguza ukatili wa kijinsia SAUT

**Na Rose Jacob,** MWANZA

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, amemwagiza katibu mkuu wa wizara hiyo, kuunda tume kuchunguza madai ya baadhi ya wahadhiri wa kiume katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine (Saut) kuwa wanawafanyia ukatili wa kijinsia na kuwasababishia kushindwa kufanya vizuri katika masomo yao.

Hatua hiyo imefikiwa kutokana na taarifa alizokuwa akizipata kutoka vyanzo mbalimbali, ikiwamo Shirikisho la Wanafunzi wa Elimu ya Juu Tanzania (Tahliso) na kumtaka Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, afike chuoni hapo kuwanusuru wanafunzi hao dhidi ya unyanyasaji huo.

Ole Nasha alifika chuoni hapo juzi kuonana na uongozi wa chuo na kukutana na Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Costa Mahalu, alikuwa ameanza tu kazi tangu kuteuliwa kushika wadhifa huo.

Baada ya kufika, Ole Nasha alifanya kikao cha ndani kisha kukutana na baadhi ya wanafunzi na uongozi wa serikali ya wanafunzi, huku akiwataka viongozi wa chuo hicho kutoka ndani ya ukumbi ili wahusika wajieleze vizuri.

Katika kikao hicho, Naibu Waziri alibaini changamoto kuu tano zinazowakabili wanafunzi, kubwa ikiwa ukatili wa kijinsia dhidi ya wanafunzi.

"Wakati wanachuo wakijieleza na uongozi wa serikali ya wanafunzi, nilibaini mambo makuu matano yanayowakabili ambayo ni ukosefu wa mifumo sahihi ambayo inatumika chuoni hapo, kuwapo baadhi ya walimu (wahadhiri) wasio waaminifu kwa kuchukua rushwa kwa wanafunzi kwa ajili ya kuwaongezea ufaulu na ukosefu wa bima ya afya ingawa wanafunzi walishalipa fedha.

"Nyingine ni ubadhirifu wa ofisa ya mikopo ya chuo na uongozi wa chuo kushindwa kutoa ushirikiano kwa wanafunzi wanapokumbwa na matatizo," alisema Ole Nasha.

Kutokana na changamoto hizo, naibu waziri aliwataka wanafunzi kuacha kuogopa kutoa ushirikiano kwa tume ambayo itafika chuoni hapo kwa ajili ya uchunguzi dhidi ya baadhi ya walimu wanaotuhumiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa na unyanyasaji wa kijinsia.

**INAENDELEA UK. 8**

# Mavunde 'apigia saluti' Total kusaidia maendeleo ya vijana

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Kazi na Vijana, Antony Mavunde, ameipongeza kampuni ya Total kwa kusaidia vijana wenye mawazo mazuri ya kibiashara na kuzitaka kampuni zingine ziige mfano huo.

Amesema kampuni hiyo imewajengea uwezo Watanzania katika kujiletea maendeleo na kuchangia maendeleo ya taifa kwa sababu serikali pekee haiwezi kufanya kila kitu, hivyo kunahitajika juhudi za pamoja kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mavunde alisema hayo juzi usiku jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya kuwatangaza washindi wa shindano la 'Total Start upper of Year' kwa mwaka huu. Katika hafla hiyo washindi watatu wa mwanzo walipatiwa tuzo na fedha taslimu zenye thamani ya Sh. milioni 75.

Alisema Total Tanzania imekuwa ikitoa misaada mbalimbali kusaidia maendeleo ya jamii ya Tanzania ikiwamo uwezeshaji wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kuwapatia mitaji na mafunzo ya kitaalamu.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Total Tanzania, Tarik Moufaddal, alisema tuzo hizo ni uthibitisho wa nia ya dhati ya Total kuwa ni mshirika wa maendeleo Tanzania na kusisitiza kuwa bado kuna mambo mengine makubwa kampuni imepanga kuwafanyia Watanzania

**INAENDELEA UK. 8**



215038602

# EU watoa mafunzo udhibiti mionzi kwa nchi 5 Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

UMOJA wa Ulaya (EU), umetoa mafunzo ya udhibiti wa uingizaji wa vyanzo vya mionzi kwa nchi tano za Afrika kwa lengo la kusaidia udhibiti wa uingizaji wa vyanzo vya mionzi bila kufuata utaratibu pamoja na utoroshwaji wa vyanzo vya mionzi vilivyoibiwa kwa matumizi yasiyo salama na hatarishi.

Washiriki wa mafunzo hayo ni kutoka taasisi mbalimbali zikiwamo Mamlaka za Mapato, Forodha na vyombo vya ulinzi na usalama kutoka katika nchi za Malawi, Rwanda, Kenya, Zambia na wenyeji Tanzania kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki.

Huu ni mwendelezo wa mafunzo kwa nchi za Afrika katika kusaidia kupambana na tabia ya uingizwaji wa vyanzo vya mionzi ambavyo kwa namna moja ama nyingine husababisha madhara kwa binadamu.

Mafunzo hayo yanahusisha vitendo ikiwamo utambuzi kwa kutumia vifaa maalumu vilivyopo katika mipaka yote katika nchi hizo na husaidia kugundua uhalifu wa namna hiyo.

Mshiriki wa mafunzo hayo kutoka Tanzania, Mhandisi Exavier Zakaria, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kwa waliopo katika mipaka na wamekuwa wakikutana na masuala mengi ikiwamo baadhi ya wafanyabiashara ambao huenda kinyume na sheria na taratibu zilizowekwa za usafrishaji wa vyanzo vya mionzi.

"Ukweli mafunzo yamekuja kwa wakati sahihi na yatasaidia sana katika kuongeza ujuzi kwenye utambuzi wa vyanzo vya mionzi ambavyo ni hatarishi kwa binadamu," alisema Mhandisi Zakaria.

Naye mshiriki mwingine wa mafunzo hayo kutoka Tanzania, Patrick Simpokolwe, alisema kutokana na mbinu za uhalifu za uingizaji wa mionzi isiyo salama katika mipaka mbalimbali Afrika, anaamini mafunzo hayo yatamsaidia katika kugundua mbinu za uhalifu na kudhibiti.

"Tumekuwa tukikumbana na udanganyifu mkubwa kwenye mipaka kutokana na mbinu mpya zinazotumiwa na wasafirishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwamo zenye vyanzo vya mionzi katakana na kuingia ndani ya nchi, hivyo mafunzo haya yatawabaini wahalifu wa

INAENDELEA UK. 8



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wa pili kulia), akikagua maabara ya chakula ya Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) wakati alipotembelea ofisi za mamlaka hiyo, Mabibo jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Meneja wa Maabara wa TFDA, Danstan Hipolite. **PICHA: OWM**

# Malumbano hoja mawakili yaweka kiporo hatima dhamana ya Mbowe

**Na Hellen Mwango**

HATIMA ya kutenguliwa uamuzi wa kuwafutia dhamana au kuendelea kukaa rumande kwa Mwenyekiti Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe na Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko itajulikana leo saa 7:00 mchana.

Hatua hiyo ilifikiwa jana na Mahakama Kuu Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam iliyoketi chini ya Jaji Sam Rumanyika baada ya kusikiliza hoja za mawakili wa pande zote mbili.

Walalamikaji kupitia mawakili Peter Kibatala na Jeremia Mtobesya kwa nyakati tofauti waliwasilisha hoja za rufani.

Katika hoja ya kwanza ya rufani, walidai kwamba Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, chini ya Hakimu Mkazi Mkuu (kwa sasa Jaji), Wilbard Mashauri, Novemba 23, mwaka jana, ilikosea kuwafutia dhamana walalamikaji.

Kibatala alidai kuwa uamuzi wa kuwafutia dhamana washtakiwa una makosa kwa sababu washtakiwa walikuwapo mahakamani Novemba 12 na 23 na kwamba walipewa nafasi ya kujieleza sababu zilizowafanya kushindwa kufika kwenye kesi yao Novemba Mosi na 8, mwaka jana.

Aidha, alidai kuwa mbali na walalamikaji kujieleza, awali wadhamini wao walifika mahakamani kueleza sababu za kukosa siku ya kesi yao.

"Mtukufu Jaji walalamikaji hawakuwapo mahakamani, lakini taarifa zilitolewa na wadhamini wao. Pia walifika mahakamani wenyewe kwenda kujieleza sababu zao. Mbowe alikwenda nje ya nchi na Matiko alitumwa kuliwakilisha bunge nje ya nchi," alidai na kuongeza:

"Tunaiomba mahakama yako itengue uamuzi wa kuwafutia dhamana walalamikaji kwa sababu Mahakama ya Kisutu ilikosea kuwafutia dhamana yao, warudi nyumbani kuendelea na maisha," alidai Kibatala.

Akiunga mkono hoja za rufani, Mtobesya alidai kuwa wadhamini wanaingia mkataba na mahakama na endapo siku mtuhumiwa asipofika, mdhamini anawajibika kutoa maelezo mahakamani kwa nini mtuhumiwa hajafika.

"Walalamikaji walikwenda mahakamani wenyewe bila hata kukamatwa, tunaomba mahakama itengue uamuzi wa Mahakama ya Kisutu washtakiwa waendelee na dhamana, wapate haki yao ya kikatiba," alidai Mtobesya.

Akijibu hoja za rufani, Wakili wa Serikali Jacqueline Nyantori, alidai kuwa walalamikaji walipewa dhamana na kufutwa kwa dhamana yao si suala la Jamhuri kuibuka mara moja.

Alidai kuwa Juni 22 na Julai 31, 2018, walalamikaji na washtakiwa wengine walionywa na Mahakama ya Kisutu kutokana na mwenendo wao wa kushindwa kufika mahakamani kusikiliza kesi yao.

"Mtukufu Jaji kati ya Julai 3, 25,

INAENDELEA UK. 8

# Hofu ongezeko la maambukizi ya VVU kisa bomba la mafuta

**Na Steven William,** MUHEZA

VIONGOZI wa asasi zisizo za kiserikali zinazojishughulisha na mapambano dhidi ya Ukimwi wilayani Muheza, wameonyesha wasiwasi wa kuongezeka maambukizi ya virusi vya ugonjwa huo (VVU) utakapoanza ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Tanga kwenda Hoima, Uganda.

Wasiwasi huo unatokana na maingiliano baina ya watu, wakiwamo wafanyakazi, kutokana na shughuli mbalimbali kwenye mradi huo.

Viongozi hao walisema hayo juzi katika mkutano uliofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ambao ulikuwa unatambulisha mradi wa Programu ya Uimarishaji wa Mifumo ya Afya na Ustawi wa Jamii, ambao pamoja na mambo mengine, unalenga kutoa elimu kwa jamii kuhusu mapambano dhidi ya Ukimwi.

Mmoja wa washiriki wa mkutano huo, Iddi Mguhi, alisema mradi huo utakuwa na wafanyakazi wengi kutoka mataifa mbalimbali, hivyo ana wasiwasi kuwa kunaweza kuongezeka maambukizi ya VVU.

Kutokana na hofu hiyo, Mguhi alisema ujenzi wa bomba hilo utakapoanza, lazima asasi zinazoshughulikia mapambano dhidi ya Ukimwi pamoja na mashirika binafsi na serikali, wapige kambi katika wilaya ya Muheza na mkoa wa Tanga kwa ujumla kwa ajili ya kutoa elimu.

Alisema kambi ya wafanyakazi wa bomba la mafuta itajengwa katika kijiji cha Tanganyika kata ya Lusanga, Muheza, hivyo kuna wasiwasi wa kuibuka kwa biashara ya ngono na vitendo vya ushoga ambavyo ni vichocheo vikubwa vya maambukizi ya VVU.

Mguhi alisema takwimu mpya zinaonyesha kwamba maambukizi ya VVU mkoa wa Tanga yameongezeka kutoka asilimia 2.4 hadi tano na kwamba zinaweza kupanda zaidi iwapo hatua hazitachukuliwa hasa katika kipindi hiki ambacho watu wengi wamekuwa wakiingia kutokana na mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta.

Alitolea mfano wa wilaya ya Muheza kuwa kiwango cha maambukizi kiko juu kutokana na mwingiliano wa watu wageni kama vile wafanyabiashara wanaochukua machungwa kupeleka Kenya.

Alisema kwa sasa katika eneo la Majengo Shimoni kuna 'madada poa' wanaojiuza na pia wako wanaume kutoka Tanga mjini wanaojihusisha na vitendo vya ushoga, hali ambayo inaongeza kasi ya maambukizi ya VVU pamoja na wanaofanya kazi katika mashamba ya chai Amani.

Naye Shabani Nyakirama, alisema katika wilaya hiyo kuna watu wanapata maambukizi ya VVU lakini hawataki kwenda kupima na wanatumia miti shamba.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Aziza Almasi, alisema kutokana na kuwapo kwa tishio hilo, halmashauri ilianza msako katika nyumba zote za kulala wageni wilayani Muheza kuangalia kama kuna wanaume watu wazima wanafanya ngono na wasichana wadogo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni fedheha wagonjwa Igunga kujisaidia kwenye nailoni

**TAARIFA** kuwa wagonjwa wanaotibiwa, wanaolazwa na watumishi wa hospitali ya Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, wanajisaidia kwenye mifuko ya plastiki na kutupa vinyesi porini au vichaka vilivyo jirani na hospitali hiyo, hazikubaliki.

Hatuzikubali kwa sababu ni aibu. Taasisi inayopaswa kuepusha watu na maradhi kugeuka kuwa mhusika mkuu wa kusambaza na kuambukiza wananchi magonjwa ni fedheha.

Kwa ujumla hii ni aibu na kwa ujumla kujisaidia huko kunakofanywa na wagonjwa na wataalamu wa afya wanawatibu kunatia doa kampeni za kupambana na adui maradhi zilizoanza tangu uhuru wa taifa hili.

Ni wazi kuwa mwenendo huo wa kuchafua mazingira ya hospitali na majirani zake kwa kinyesi unasababisha milipuko ya magonjwa ya kuhara kama kipindupindu, kuhara damu, homa ya matumbo na minyoo kwa wanadamu na hata wanyama.

Taarifa za kwamba wateja na watumishi wa hospitali hiyo wanajisaidia porini zilichapishwa jana na gazeti hili zikiwanukuu wagonjwa, jamaa zao na viongozi wa hospitali zikisema kuwa wanajisaidia kwenye mifuko na kutupa vinyesi porini kwa sababu choo kimejaa na kimefungwa.

Kaimu Ofisa Afya wa Wilaya ya Igunga, Andrew Ndomondo, anakiririwa akisema vyoo hospitalini vimefungwa na kwamba ni kwa muda mrefu hakuna vyoo na kwamba, uongozi umetoa taarifa, lakini hakuna kilichofanyika.

Tunaomba kuwaeleza wananchi na uongozi wa hospitali hiyo kuwa kwenda haja ovyo pengine mashambani, porini, vichakani, msituni , mtoni, ziwani na baharini badala ya kutumia vyoo kunaleta magonjwa na kuhatarisha maisha.

Kujisaidia porini kunaeneza magonjwa kwa watu wengi na kunachafua mazingira. Kwa mfano, kinyesi cha binadamu kusombwa na maji wakati wa mvua na kupelekwa sehemu mbalimbali, iwe mtoni na kwenye bustani za mboga kunaeneza magonjwa mengi. Maji kwa mfano, yakichafuka na kinyesi wote tunafahamu kuwa uchafu huo una wadudu na vimelea vya maradhi ambavyo vinadhuru na yanaponywewa na binadamu au wanyama ni hatari kwa maisha ya kila mtumiaji.

Kinachotokea kwenye hospitali ya Igunga si jambo la kupuuzwa, ni lazima hatua zichukuliwe kuokoa maisha ya wagonjwa, watumishi wa serikali na majirani wanaopokea mizigo ya vinyesi na haja ndogo inayotupwa kwenye mashamba na makazi yao.

Tunapenda kutoa msisitizo kwa serikali mkoani Tabora na wilayani Igunga kuwa zama zimebadilika. Ni wakati wa kubadilisha miundombinu ya vyoo vyetu na kujenga choo cha maji ambacho ni rahisi kukihudumia kinapojaa badala ya choo cha shimo ambacho hulazimisha kukifunga na kuchimba jingine.

Tunazikumbusha serikali hizo kuwa pamoja na kufanya jitihada nyingi za kuboresha maisha ya wananchi hasa wanyonge na hili pia ni jukumu lake kuonyesha dhamira ya dhati ya kupambana na tatizo hilo ambalo liko sehemu nyingi nchini.

Pamoja na kujenga vyoo na miundombinu ya huduma za choo kama mifumo ya kuondoa na kuzoa maji taka hospitalini hapo na kuweka tanuru la kuchoma taka za hospitalini Igunga, serikali ya mkoa huo iendelee na kampeni za kuwahamasisha wananchi kufahamu na kukwepa athari za kujisaidia vichakani kwani ni njia ya kusambaza magonjwa na kudhoofisha zao.

Aidha tunachukua fursa hii kuwakumbusha wabunge wetu kuwa serikali yetu inatoa fedha za kusaidia maendeleo ya jimbo hivyo wakumbuke kuwa ni jukumu lao kama viongozi kutumia fedha walizonazo kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya majimbo yao. Tunawaomba kushiriki kuhamasisha maendeleo ya wapiga kura wao ikiwa ni pamoja na kujenga huduma muhimu kama vyoo vya hospitalini na shuleni.


Shime tushirikiane kumaliza tatizo hili linalotishia afya za Watanzania wa Igunga.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hoja hii ya usafi, kujali watoto tuungane nao viongozi wa dini

Na Salome Kitomari

**JUZI** viongozi wa dini nchini, walitoa tamko la kukubali kushirikiana na serikali kukabiliana na ulinzi na usafi wa mazingira kwa watoto, kutokana na madhara yanayoendelea kuwapo.

Makubaliano yao ni kwenda kuwahamasisha waumini kupitia mahubiri, ili wafahamu umuhimu wa kulinda watoto na kuishi katika hali ya usafi wakati wote, kuwaepusha watoto na matatizo ya afya, kama kudumaa katika makuzi yao.

Muungano huu ni mzuri, kwa kuwa unagusa afya za wananchi moja kwa moja na kwenye nyumba za ibada, ndiko ambako wanapaamini, wanasikia na kutii sauti za viongozi wao. Maana yake, sasa tutarajie mabadiliko makubwa.

Hakuna ubishi, lipo tatizo kubwa la usafi wa mazingira kwenye mitaa mbalimbali ya miji mkubwa na mdogp. ambalo kwa kiasi kikubwa, limesababishwa na watu kushindwa kutekeleza wajibu wao na ukosefu wa miundombinu bora ya kuhifadhia taka, kupitisha na kuteketeza taka hizo.

Kauli ya viongozi wa dini katika kupaza sauti, itakuwa na nguvu zaidi, iwapo tu watashirikiana na mamlaka za kiserikali. Vinginevyo, hali itaendelea kuwa ile ile, kwa kuwa wakati mwingine, utatuzi huo unahitaji nguvu ya serikali.

Mathalani, masoko ya jiji la Dar es Salaam, ni chanzo cha uchafu na uondoshaji wa taka haufanyiki inavyotakiwa, huku kukiwa na sababu mbalimbali ambazo kimsingi siyo za msingi sana. Mfano katika kila soko wachuuzi hulipa ushuru wa Sh. 500 kila siku na wapo wakusanyaji wa fedha hizo ambazo huenda Manispaa ambazo wakati mwingine mapato ya soko hufikia Sh. bilioni moja kwa mwezi, lakini fedha inayotengwa katika kuondosha takataka ni ndogo sana na wakati mwingine hakuna. Kwa ujumla masoko ni machafu sana, magari ya takataka ambayo yalitakiwa kuwapo kila siku hukosekana hata kwa wiki moja na matokeo yake taka kuwa nyingi, mbaya zaidi kazi hiyo inafanywa na manispaa zenyewe. Ukitembelea baadhi ya masoko, utajiuliza kwanini hali inaendelea kuwa hivi kwa kuwa kuna uchafu mwingi ambao siyo salama kwa afya za wauzaji na wanunuzi? Hakuna miundombinu muhimu na hakuna jitihada za haraka katika kuhakikisha masoko, yanakuwa ni sehemu salama.

Kwenye masoko hayo kuna watoto ambao wameambatana na mama zao kusaka riziki ya siku, moja kwa moja wanajikuta kwenye mazingira hatarishi na usalama wa afya zao upo hatarini. Kwa ujumla, matamko ya viongozi wa dini liende sambamba na Manispaa kuchukua hatua ya kuleta mabadiliko kwenye masoko, yanayobeba mamilioni ya watu wakiwa wanunuzi na wakati huohuo wauzaji.

Eneo jingine ni uondoshaji wa takataka kwenye mitaa mbalimbali ambalo limeonekana kushindwa licha ya mbinu mbalimbali kutumika ikiwamo kutumia vijana maalum kukamata wanaochafua mazingira.

Mitaani, hakuna magari ya kuondosha takataka, matokeo yake takataka zinazozalishwa hutupwa sehemu mbalimbali nyakati za usiku, na hakuna jitihada za serikali za mitaa kuhamasisha wananchi kuchanga kwa ajili ya gari au wabeba taka.

Kama uondoshaji wa takataka kwenye nyumba za watu unashindikana na muumini huyu ndiye aliyekutana na mahubiri ya kiongozi wa dini akimataka kushiriki usafi wa mazingira katika kulinda afya za watoto, lakini hakuna pa kuhifadhi takataka bali zinazagaa.

Kwenye maeneo yenye taka, ndiko ambako watoto hupita au kucheza, hivyo kuokota ambavyo kwa uwezo wa akili zao wanaona vinafaa, lakini kiuhalisia ni hatari kwa afya zao. Manispaa ya Moshi inahesabu mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika usafi wa mzingira kwa kuwa wameshirikiana kwa pamoja na Manispaa, mamlaka za serikali,viongozi wa dini, siasa na wananchi kusema hapana kwenye uchafu.

Wasifu kama huo wa usafi nao unaonekana kwa miaka mingi, katika Manispaa ya Iringa.

Mara nyingi, nimezuisikia manispaa na mamlaka nyingine za miji, zikienda huku kujifunza ili kuboresha na hata Manispaa za Dar es Salaam zilishakwenda kujifunza, lakini bado mabadiliko hayajaonekana, bali tunaona nyakati za mvua watu wanatoa mafurushi ya taka kwenda kurusha kwenye mitaro.

Eneo jingine ni chemba za majitaka ambazo mara nyingi hutiririsha majitaka kwa muda mrefu, jambo linaloleta madhara ya afya, kama mlipuko wa kipindupindu na magonjwa mengine. Uamuzi wa viongozi wa dini unapaswa uungwe mkono, ili kuhakikisha serikali na wananchi wanakuwa kitu kimoja, kuhakikisha usafi wa mazingira ni utamaduni ya kila mmoja, kama ilivyowezekana Manispaa ya Moshi na kwingine itawezekana.

## HABARI KITAIFA

# Watoto wenye uhitaji wapewa vifaa vya zaidi ya mil. 9/-

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, wafanyakazi wa kampuni ya mawasiliano ya Vodacom Tanzania Plc., kupitia mpango wake wa Pamoja na Vodacom ulio chini ya taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation, jana wamechangia vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 9.6 kwa kituo cha watoto wenye uhitaji maalum cha Mwanangu Special Kilichopo Mkuranga, mkoani Pwani.

Kituo hicho kina jumla ya watoto 40 kati yao 20 ni wenye mahitaji maalum kama mgongo wazi, vichwa vikubwa na 'down syndrome'.

Wafanyakazi hao walitoa vifaa; viti maalum, magongo ya kutembelea, magongo ya kusimamia, mashine za uzito, viatu 'Special Orthopedics', vitanda vya watoto wenye ulemavu na mashine za kufulia.

Mbali na misaada hiyo, wafanyakazi hao pia walicheza na kufurahi pamoja na watoto hao kwa ajili ya kuwapatia faraja.

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga, aliipongeza kampuni ya Vodacom kwa mpango huo na kusema serikali imedhamiria kuboresha maisha ya kila Mtanzania ili kutimiza dira ya maendeleo ya taifa na jitihada kama hizo kutoka kampuni binafsi zinazosaidia serikali kutimiza malengo yake.

Alisema msaada huo utasaidia kuhudumia watoto wenye ulemavu nchini na kuhimiza taasisi zingine kufuata nyayo za Vodacom. Mpango wa pamoja na Vodacom umekuwa ukitumiwa na wafanyakazi wa kampuni hiyo ili kurejesha fadhila kwa jamii. Mpango huo umewafanya wafanyakazi wa kampuni hiyo kuwa mawakala wa mabadiliko kwa kusaidia kutatua changamoto zilizopo katika jamii.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Vodacom Tanzania, Jacquiline Materu, alisema wafanyakazi wa kampuni hiyo wanashauku ya kuisaidia jamii na huo ni utaratibu wao kwa miaka zaidi ya 12 kupitia Vodacom Tanzania Foundation.

"Katika kusherehekea wiki hii ya wanawake duniani, tumeona ni vyema kusherehekea na wadogo zetu, kuwapatia mahitaji muhimu na pia kuwawezesha kuwa na nyenzo muhimu za kuwasaidia kufikia ndoto zao kwa kuwa ulemavu sio kikwazo cha mafanikio," alisema.

# Exim kuinunua Benki ya UBTL

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim Tanzania imezidi kujiimarisha baada ya kuonyesha nia na utayari wa kuinunua rasmi Benki ya UBL Tanzania Limited (UBTL) kwa asilimia 100.

Hatua hiyo inafuatia baada ya kusaini barua ya kuonyesha nia ya kufanya hivyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana jijini Dar es Salaam na Naibu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu, ununuzi huo unaohusisha mali na madeni unazidi kuifanya benki hiyo ambayo kwa sasa ni miongoni mwa benki tano kwa ukubwa nchini, kuzidi kujitanua ndani na nje ya nchi.

"Kwetu ni furaha kubwa kuona kwamba familia yetu inazidi kuongezeka kwa kuwa tayari tunaungana na wanafamilia kutoka Benki ya UBTL. Zaidi ya yote tunaamini pia kuwa wafanyakazi wa Benki ya UBTL wataongeza nguvu ambayo kwa pamoja tutaweza kutoa huduma bora zaidi za kibenki kwa wateja wa UBTL," alisema Matundu.

Alisema wanatarajia kukaribisha wateja wa Benki ya UBTL katika mtandao mpana wa matawi ya Benki ya Exim, huku akiongeza kuwa hatua ya ununuzi huo ni upanuzi wa asili na uimarishaji wa uwapo wa benki hiyo katika soko la ndani ya nchi.

Kwa upande wake Ofisa Mtendaji Mkuu wa UBTL, Gasper Njuu, alisema benki hiyo pamoja na wanahisa wake wamekuwa na mtazamo chanya kuhusu fursa za ukuaji nchini na kwa sasa hilo linakwenda kufanikiwa kupitia Benki ya Exim.

"Wakati tukiwa kwenye mkakati wa mabadiliko ya kibiashara kupitia uwekezaji zaidi kwenye huduma za kidijitali ndipo tulipokea ombi kutoka Benki ya Exim wakiomba kununua UBTL na baada ya kufikiria kwa kina pande zote wakiwamo wanahisa wetu, walikubaliana na ombi hilo hasa kwa kuzingatia ubora, weledi na sifa za Benki ya Exim kwa hapa nchini ambao kimsingi unaleta tija kubwa kwa wadau na wateja wetu," alibainisha Njuu.

Alisema hatua ya ununuzi inahusisha taratibu kadhaa za kisheria zikihusisha nchi za Tanzania na Pakistan na zinatarajiwa kukamilika katikati ya mwaka 2019.

Benki ya UBTL ilianzishwa mwaka 2013, kama benki tanzu inayomilikiwa na Benki ya United Bank Limited (UBL) ambayo ni ya pili kwa ukubwa nchini Pakistan na imetoa huduma za kibenki za rejareja na za jumla kwa wateja mbalimbali.




TANZANIA CHAMBER OF MINERALS AND ENERGY

TAARIFA KWA UMMA

KUBADILISHWA KWA JINA

Tangazo hili linatolewa kuujulisha umma kwamba taasisi ya Tanzania Chamber of Minerals and Energy (TCME) imebadilishwa jina pamoja na nembo yake. Maelezo mengine yote kuhusu taasisi hii ikiwamo anuani, vyeo pamoja na majina ya watendaji wake yanabaki kama yalivyokuwa hapo awali. Kufuatia mabadiliko hayo:

Jina jipya litakuwa ni:

TANZANIA CHAMBER OF MINES

Nembo (kuu) mpya itakuwa ni: Tanzania Chamber of Mines "Mining for National Development"

Nembo (ndogo) mpya itakuwa ni: TCM

Kuhusu Tanzania Chamber of Mines

Tanzania Chamber of Mines (TCM) ni taasisi binafsi na ya hiyari iliyoundwa mwaka 1994. Inawakilisha makampuni wanachama kutoka sekta rasmi ya uchimbaji madini, kuanzia watafiti wadogo hadi wazalishaji wakubwa, pamoja na wachimbaji wa kati na watoa huduma. Taasisi inawawakilisha kwa sauti moja wanachama wake katika kuleta mahusiano bora kati ya kampuni zilizowekeza katika sekta ya madini na Serikali, pamoja na wadau wengine wakiwamo jamii pamoja asasi za kiraia zinazojihusisha na rasilimali madini.

Taasisi pamoja na wanachama wake tunaunga mkono mfumo bora wa uchimbaji madini na unaoratibiwa vema, huku tukiweka msisitizo katika kuhakikisha kwamba wanachama wetu wanatii sheria za nchi na za kimataifa katika kudhibiti masuala ya ulipaji kodi, utunzaji wa mazingira pamoja na usalama kazini.

Anuani: S. L. B. 13369; Kiwanja Na.8 Barabara ya Manara Road, Ada Estate, Wilayaya Kinondoni, Dar es Salaam, Tanzania.

Simu +255 22 2 667594 Fax: +255 22 2 667511 Parua pepe: info@chamberofmines.org Wavuti: www.tcme.or.tz

Imetolewa na
Mwenyekiti
Tanzania Chamber of Mines

215098002



Aliyekuwa kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Hamis Mgeja, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, juu ya nia yake ya kurudi katika chama chake cha awali CCM. Kushoto ni kada wa CCM, Abeis Abeid. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Malumbano hoja mawakili yaweka kiporo

INATOKA UK. 4

31 na Agosti 2, 2018, walalamikiwa kwa nyakati hizo tofauti walionywa kwa tabia yao ya kutokufika mahakamani wakasababisha kesi kusimama kuendelea kusikilizwa," alidai.

Pia alidai kuwa Novemba Mosi, mwaka jana, upande wa Jamhuri ulishindwa kuvumilia na uliibua hoja ya kuiomba mahakama kutoa hati ya kukamatwa washtakiwa.

Nyantori alidai kuwa Novemba 8 mahakama ilikubali kutoa hati ya kukamatwa na walalamikaji walijisalimisha mahakamani Novemba 12, 2018 siku nne baadaye.

"Mtukufu Jaji dhamana ilifutwa kwa nia nzuri ili kesi iendelee kusikilizwa kwa sababu kulikuwa na ucheleweshaji wa makusudi," alidai wakili huyo wa Jamhuri.

Hata hivyo, alidai kuwa kabla ya dhamana kufutwa wadhamini waliitwa kujieleza na waliiambia mahakama sababu ambazo ilizitathmini ikaona hazina msingi.

Alidai kuwa sababu za wadhamini zilikuwa zinajichanganya na kwamba mahakama ilibaini walalamikaji wamekiuka na kuvunja masharti ya dhamana, hivyo walijiondolea haki yao ya dhamana.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya jaji na wakili wa serikali;-

**Jaji:** Natamani kujua walalamikaji walikamatwa au walikuwa hawakamatiki?

**Wakili:** Mtukufu Jaji zilitolewa taarifa, Mbowe alikuwa nje ya nchi na mshtakiwa wa tano ambaye hapa ni mlalamikiwa wa pili.

**Jaji:** Dhamana ilifutwa siku hiyo walipofika?

**Wakili:** Hapana mtukufu jaji siku hiyo walipewa haki ya kusikilizwa na mahakama ndipo uamuzi ukatolewa.

Jaji Rumanyika alisema, amesikiliza hoja za pande zote mbili na mahakama yake itatoa hukumu leo saa 7:00 mchana.

Wiki iliyopita Mahakama ya Rufani ilitupilia mbali rufani ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ya kupinga Mbowe na mwenzake kusikilizwa na Mahakama Kuu.

Mbowe na Matiko kwa pamoja wamekata rufani wakipinga kutenguliwa kwa dhamana yao na Hakimu Mkazi Mkuu, (kwa sasa Jaji wa Mahakama Kuu) Wilbard Mashauri.

Katika maombi yao walalamikaji wanadai kwamba Mahakama ya Kisutu ilikosea kufuta dhamana kwa washtakiwa wakati wao wenyewe walifika mahakamani Novemba 12, 2018 na Novemba 23, 2018, pia walihudhuria mahakamani siku dhamana yao ilipofutwa.

Novemba 23, 2018, Mahakama ya Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mashauri iliwafutia dhamana Mbowe na Matiko baada ya kushindwa kufika mahakamani kusikiliza kesi yao ilipopangwa kati ya Novemba Mosi na 8, mwaka huu.

Hakimu alisema Novemba Mosi, mdhamini wa Mbowe alidai mahakamani kwamba ameugua ghafla yuko mahututi hawezi kuongea na amepelekwa kutibiwa nje ya nchi.

Pia wakili wa utetezi, Peter Kibatala, alidai kuwa mshtakiwa ni mgonjwa mahututi amepelekwa nchini Afrika ya Kusini.

Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi, alipinga sababu zilizotolewa na utetezi na kuiomba mahakama kuamuru utetezi kuwasilisha vielelezo kuhusu maradhi ya Mbowe.

Mahakama iliamuru washtakiwa wakamatwe na kufikishwa mahakamani kujieleza kwanini wasifutiwe dhamana. Novemba 12, Mbowe na Matiko walijisalimisha mahakamani.

Mbowe wakati akijitetea ili asifutiwe dhamana alidai kuwa aliondoka nchini Oktoba 28, mwaka jana, kwenda Marekani na alianza kuugua akiwa huko Oktoba 31.

Alidai kuwa Novemba 2, alikwenda nchini Ubelgiji wakati akisubiri ahadi ya kuonana na daktari wake Novemba 8 na kwamba alishauriwa asisafiri mwendo mrefu akiwa angani.

Kwa upande wake, Matiko alidai kuwa alishindwa kufika mahakamani kwa sababu alihudhuria mkutano wa michezo kwa mabunge ya Afrika Mashariki akiiwakirisha Tanzania.

"Kwa kuwa mshtakiwa wa kwanza taarifa zake zinakinzana, hati yake ya kusafiria inatofautiana na maelezo yake, mshtakiwa wa tano pia sababu zake hazina mashiko, mahakama yangu inawafutia dhamana kuanzia leo," alisema Hakimu Mashauri.

Katika kesi ya msingi, mbali na Mbowe na Matiko, washtakiwa wengine ni Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Mbunge wa Kawe Halima Mdee; Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya; na Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji.

Washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 13, ikiwamo kula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia, kuhamasisha hisia za chuki, kushawishi hali ya kutoridhika, uchochezi na kushawishi utendaji wa kosa la jinai kati ya Februari 1 na 16, mwaka jana jijini Dar es Salaam.

# Tume kuundwa

INATOKA UK. 3

Pia alimtaka Makamu Mkuu wa Chuo kuhakikisha mtu yeyote atakeyetoa ushahidi dhidi ya watuhumiwa, hapati matatizo kwa namna yoyote.

Sambamba na hilo, aliagiza uchunguzi ufanyike dhidi ya mifumo ya chuo hicho kutokana na kuingiliwa na watumishi ambao wamekuwa wakifanya biashara haramu ya uuzaji wa matokeo, jambo linalosababisha kupatikana wahitimu wasio na sifa.

Alisema iwapo itabainika wanafunzi wote walimaliza katika chuo hicho ambao waliongezewa ufaulu, watafutiwa matokeo na mhadhiri aliyehusika atafukuzwa kazi na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Naye Mwenyekiti wa Tahliso, Peter Niomboye, aliomba serikali kuhakikisha uchunguzi huo unafanyika kwa kina kutokana na ushahidi kuwapo wa kutosha.

"Sisi Tahliso tunaiomba serikali itakapokamilisha uchunguzi wake, ihakikishe mtuhumiwa mmoja ambaye baada ya suala lake la ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi chuoni hapa kubainika, alikimbia nchini na kwenda kusoma nje ya nchi, hivyo endapo atabainika basi arudishwe nchini ili ajibu tuhuma zinazomkabili.

Prof. Mahalu alimhakikishia naibu waziri kuwa katika uongozi wake hatakubaliana na maadili machafu kwa watumishi wa chuo hicho, ambao wanategemewa kutengeneza vijana watakaokuwa na faida kubwa ya taifa halafu mtumishi ndiye anakuwa daraja la uharibifu, jambo hilo hatulikubali kabisa.

# Mavunde 'apigia saluti' Total

INATOKA UK. 3

katika kuchangia maendeleo.

Washindi hao kwa upande wao, waliishukuru kampuni ya Total kwa kutambua vipaji vyao, hivyo kuwapatia zawadi watakazozitumia kuboresha miradi yao.

Mshindi wa kwanza ni Doreen Noni, aliyepata tuzo na fedha taslimu Sh. milioni 30 kwa wazo la uanzishaji kipindi cha TV kinachoitwa 'Peter's Daughter Show' kwa lengo la kusaidia vijana kukabiliana na changamoto mbalimbali za maendeleo, ikiwamo tatizo kubwa la msongo wa mawazo kwa vijana walioshindwa kufanikiwa.

Michael Sayi, alibuka mshindi wa pili kwa kupewa tuzo na Sh. milioni 20 kwa mradi wa Kasome International unaowasaidia wanafunzi wa shule za sekondari Tanzania, kujipatia vitabu na masomo ya ziada kupitia mtandao, hivyo kupunguza gharama kwa wanafunzi kutoka familia maskini kupata mafunzo bora kwa gharama ndogo.

Mshindi wa tatu ni Prince Tillya aliyepata tuzo na fedha taslimu Sh. milioni 15 kwa mradi wake wa FixChap, unaounganisha mafundi bora wa huduma mbalimbali za nyumbani kwa gharama nafuu.

# EU watoa mafunzo udhibiti

INATOKA UK. 4

namna hiyo," alisema Simpokolwe.

Mshiriki kutoka Kenya, Evalyne Rotich, alisema kutokana na uwezekano wa kutokea uhalifu kila wakati, mafunzo hayo yatawezesha kutambua watu ambao sio wema wenye lengo la kupitisha vitu vyenye vyanzo vya mionzi mipakani ambavyo vinaweza kudhuru wananchi katika nchi husika.

"Umakini utaongezeka kwetu kwa kuwa mbinu tulizopatiwa zitatuwezesha kutambua vitu vyote ambavyo vitapitishwa bila kufuata utaratibu husika,"alisema Rotich.

Mmoja wa wakufunzi wa mafunzo hayo kutoka umoja wa Ulaya, Katrijin Vandersteen, alisema katika nchi za Afrika kumekuwa na tatizo la uingizaji wa vyanzo vya mionzi visivyo salama hivyo kutolewa kwa mafunzo hayo kutasaidia uimarishaji wa utambuzi na udhibiti katika maeneo ya mipaka kwenye nchi mbalimbali.

"Tunaamini kuwa washiriki hawa watapata uelewa zaidi juu ya utambuzi wa vyanzo vya mionzi visivyo salama kwa kusaidia kutoleta madhara kwa binadamu kwenye nchi husika na dunia kwa ujumla baada ya kukamilika kwa mafunzo haya," alisema Vandersteen.

Mafunzo hayo yanaendelea Makao Makuu ya Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, jijini Arusha, yalianza Machi 4 na yanatarajiwa kumalizika kesho.

HABARI KITAIFA

# Hasunga, Tulia wajitosa sakata la wakulima viazi

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga na Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, wamejitosa kushughulikia kero sugu zinazowakabili wakulima wa viazi mviringo mkoani Mbeya.

Kero zinazowakabili wakulima hao ni pamoja na faini zisizo rafiki za vifungashio, ufungaji wa mifuko (zipu) wakati wa kusafirisha, usumbufu wa mawakala wa kilimo wakati wa kusafirisha viazi na sheria ya vipimo kutokuwa rafiki kwa kuwa viazi hutofautiana uzito kutokana na msimu.

Kero nyingine ni rushwa kwa baadhi ya watumishi wa masuala ya viwango na mizani, hususan katika vituo vya ukaguzi visivyo rasmi vilivyoko Makambako, Iringa, Morogoro, Mikese na Kibaha.

Katika taarifa iliyosomwa na wakulima hao juzi mbele ya Waziri Hasunga na Naibu Spika, wakulima hao waliomba serikali kutatua changamoto hizo ambazo kwa muda mrefu zimekuwa kero bila kupatiwa majibu. Hasunga alisema serikali imedhamiria kwa dhati kutatua kero zisizo rafiki kwa wakulima na Watanzania wote, hivyo kero hizo zitashughulikiwa.

"Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwenye zao hili muhimu la viazi mviringo nami niwaahidi kutekeleza kwa haraka kadhia hii inayowasumbua," alisema Hasunga. Pia aliwaeleza wakulima hao waliojitokeza katika mkutano huo kuwa wizara yake imejipanga kuhakikisha wakulima wote nchini wanasajiliwa ili kubaini kiwango cha mashamba wanayolima na uwezo wa uzalishaji wa mazao.

Vilevile alisema serikali imeanza mkakati wa kuwa na bima ya mazao kwa kuwa kufanya hivyo wakulima watakuwa na ahueni pindi yanapotokea majanga katika mazao wanayolima.

Naye Naibu Spika aliwapongeza wakulima hao wa viazi mviringo kwa kuwa wavumilivu wakati serikali inatafuta ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili.

Alisema Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara zitakutana kutatua kadhia hizo ili wakulima mkoani Mbeya na mikoa mingine nchini wazalishe na kusafirisha mazao yao pasina vikwazo vyovyote.




Mwanzilishi wa kampuni ya kimataifa ya huduma za Bima ya Howden (kulia) iliyopo chini ya kampuni mama ya Hyperion Insurance Group, David Howden, akiongea na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa kampuni ya Howden Puri Insurance Brokers nchini, uliofanyika jijini Dar es Salaam jana, wengine pichani (kutoka kulia) ni Balozi wa Uingereza nchini, Sarah Cooke, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Howden Puri, Umesh Puri na Mwenyekiti wa Howden Kanda ya Afrika, Pravceen Vashista. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Muheza, kampuni ya Ujerumani kuwekeza mkonge

**Na Boniface Gideon,** MUHEZA

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Nassib Mmbaga, amesema halmashauri hiyo iko kwenye makubaliano na kampuni ya Agritek kutoka Ujerumani kwa ajili ya kuingia mkataba utakaowawezesha kuwa na shamba la pamoja la mkonge lenye ukubwa wa hekta 2,000.

Uwekezaji huo unatarajiwa kufanyika katika eneo la Kibaranga lenye hekta 5,000 ambalo sehemu yake itagawiwa kwa wananchi na eneo litakalobaki litafanyika uwekezaji huo wa viwanda ambao unatarajiwa kutoa ajira kwa watu wengi.

Mmbaga alisema juzi kwamba kwa sasa halmashauri na kampuni hiyo wako katika hatua za awali za maandalizi ya mkataba huo ambao utakuwa na lengo la umiliki wa pamoja wa shamba hilo.

Alisema umiliki wa shamba hilo ni kwa ajili ya kuendesha kiwanda cha katani ambacho kitakuwa chini ya halmashauri na Agritec.

Kwa mujibu wa Mmbaga, halmashauri ina mali za kuendesha kiwanda hicho ikiwamo Korona ambazo tayari wameshazifanyia uthamini na Jiji la Tanga linaendelea kufanyia kazi hiyo ili kupata thamani halisi.

"Tunasubiri tumalize uthamini na mtathmini mkuu wa serikali ili tumalize huu mkataba ambao halmashauri itakuwa inapata gawio la asilimia 51, huku mwekezaji akipata asilimia 49 lakini mwisho wa siku ile mali inabaki kuwa ya halmashauri pindi mkataba utakapomalizika," alisema.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Muheza, Balozi Adadi Rajabu, alisema katika matokeo ya kidato cha nne, mkoa wa Tanga kwa ujumla haukufanya vizuri, hivyo iko haja ya kuendelea kuweka mikakati ya kuondokana na hali hiyo.

Adadi alisema wanaishukuru serikali kwa kutoa fedha za kujengea vyumba vya madarasa na madawati na kwamba Muheza imepata fedha nyingi kwa ajili ya kusaidia sekta ya elimu.

Alisema ni juhudi zao kuhakikisha wanajenga kwa haraka madarasa hayo ili wanafunzi ambao hawajapata nafasi waanze masomo.

Adadi alitoa mfano kwa Wilaya ya Pangani ambayo iliweka mikakati na hatimaye kufanya vizuri katika matokeo kidato cha nne kwa kushika nafasi ya 50 kitaifa na namba moja kimkoa.

# Mpango waanza wagonjwa NHIF kutibiwa Aga Khan

**Na Beatrice Shayo**

MTANDAO wa Mashirika ya Maendeleo ya Aga Khan (AKDN) umesema uko katika mazungumza na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ili kuwawezesha wenye bima hiyo kupata huduma katika hospitali zilizo chini ya taasisi hiyo.

Mkurugenzi wa Tiba na Afya wa Taasisi ya Huduma za Afya Aga Khan Tanzania, Dk. Ahmed Jusabani, alisema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusiana na uzinduzi wa jengo jipya lililogharimu Sh. bilioni 192 lililoko katika Hospitali ya Aga Khan.

Alisema Hospitali ya Aga Khan ilikuwa inapokewa wagonjwa wa bima ya NHIF hadi mwaka 2012 lilipotokea tatizo na kushindwa kuendelea kutoa huduma kwa wenye bima hiyo.

"Baada ya hapo tulianza tena kuwapatia huduma na mwaka jana wagonjwa 300,000 walipatiwa huduma ya bima ya NHIF katika vituo vyetu zaidi ya 20 vilivyoko Dar es Salaam na mikoa mingine. Kwa Dar es Salaam tunaendelea kuwapokea wagonjwa ambao ni wabunge. Si kwamba tumekataa kupokea bima hiyo bali tuko kwenye majadiliano na bodi ya NHIF," alisema.

Alisema fikra iliyopo kwa sasa ni kila mmoja kupata huduma katika hospitali ya Aga Khan na wanachokiangalia ni mfumo wa rufani ili wale wanaostahili kufika wapate huduma.

Pia alisema wanaendelea kutoa kwa wenye bima ya NHIF na kwa mwaka huu wanatarajia idadi ya wagonjwa kuongezeka, huku wakiendelea na mazungumzo na bodi.

Aidha, alisema hospitali hiyo haina gharama kubwa ikilinganishwa na zile zinazotolewa nje ya nchi na mkakati wao ni kuhakikisha huduma zao zinawafikia wananchi wote.

Dk. Jusabani alisema kuna programu ambazo wameziweka katika hospitali hiyo ili wananchi wasiende nje ya nchi kutokana na gharama za nje ya nchi kuwa kubwa.

Aidha, alisema jengo hilo jipya litazinduliwa Machi 9, mwaka huu, na Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, ikiwa ni sehemu ya kuongeza huduma za matibabu.

# Kigoma, Mtwara vinara noti chafu

**Na Margret Magoso,** KIGOMA

MIKOA ya Kigoma na Mtwara ni vinara katika uchafuzi wa fedha za noti, hali inayoigharimu serikali kutumia fedha nyingi katika kuchakata fedha hizo, imeelezwa.

Akizungumza juzi mjini hapa kwenye elimu elekezi juu ya utunzaji wa fedha za noti, Meneja Msaidizi kutoka Idara ya Umma ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Vicky Msina, alisema uchafuzi huo umeifanya serikali kutoa elimu kwa jamii namna ya utunzaji wa fedha kwa maendeleo ya taifa kwa ujumla.

"Mikoa hii ni shida katika suala zima la uhifadhi na utunzaji wa fedha. Kigoma inaongoza kwa kuchafuka noti huku ikifuatiwa na Mtwara. Kila mwaka zikija kwetu zinakuwa chakavu, hiki ni kiashiria cha utunzaji na uhifadhi duni kutoka kwa raia.

"Sasa leo (juzi) mnaelimishwa, badilikeni na tumieni pochi na msikunjekunje kwenye pindo za nguo. Usafi ni muhimu kwenye kushika fedha," alisema.

Pamoja na elimu hiyo, wananchi walioshiriki walinufaika na faida za kutambua alama za noti bandia ili kuepuka uingizaji wa noti hizo katika mzunguko wa fedha na mikoa iliyoko mipakani ni waathiriwa wakubwa wa noti bandia.

Fidelis Mkate, mchambuzi wa mambo ya fedha, alisema wajasiriamali pamoja na kampuni binafsi watumie fursa ya kuikopesha serikali kuanzia Sh. 500,000 hadi milioni moja kwa lengo la kuendeleza miradi ya serikali katika nyanja tofauti.

Mwenyekiti wa wauza mikaa mkoani Kigoma, Fadhili Kiswaga, akiri uchafu na uchakavu wa noti unachangiwa na utunzaji mbovu sambamba na biashara husika.

Kiswaga alitolea mfano wauza mkaa ambao wengi ni kinamama, huzikunja noti zaidi ya mara nane na hufunga kwenye pindo la kanga huku wachache wakihifadhi kwenye mikoba.

Elimu hiyo imetolewa kwa viongozi wa serikali, wafanyabiashara na wanasiasa kwa nia ya kuwajengea ufahamu wa utunzaji na uhifadhi wa noti sambamba na utambuzi wa noti bandia.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, akifurahia jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Taifa ya Biashara NBC, Theobald Sabi (kulia), pamoja na Meneja Uhusiano wa NBC, William Kallaghe, walipokwenda kumtembelea ofisini kwake Ilala Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mafuta ya kula ya magendo yanaswa

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

NDOO 16 za ujazo wa lita 10 kila moja za mafuta ya kula zimekamatwa wilayani Masasi mkoani Mtwara, zikitokea nchini Msumbiji kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwamo ya kibiashara nchini.

Mafuta hayo yalikamatwa juzi usiku wa manane katika kijiji cha Chipingo, Tarafa ya Mchaulu wilayani Masasi. Kijiji hicho kiko mpakani kati ya Tanzania na Msumbiji.

Bidhaa hiyo ilikamatwa kutokana na uongozi wa tarafa hiyo baada ya kuwawekea mtego watu ambao walikuwa wakiyasafirisha.

Akizungumzia tukio hilo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee, Katibu Tawala wa Wilaya, Mohamed Azizi, alisema mafuta hayo yalikuwa yakivushwa kutoka Msumbiji na kuingizwa Tanzania.

Alisema baada ya kupata taarifa, ofisi ya mkuu wa wilaya kupitia katibu tarafa kwa kushirikiana na mgambo wa kata na vijiji, waliweka mtego na hatimaye kukamata shehena hiyo.

Katibu tawala huyo alisema mafuta hayo yalikamatwa katika kijiji cha Chipingo kilichoko mpakani kwa Msumbiji na Tanzania na kwamba yalikuwa yakipelekwa Newala na Masasi kwa ajili ya kuuzwa. Azizi alisema licha ya mhusika kukamatwa na ndoo hizo, pia alikuwa akijaribu kukwepa kulipa ushuru, hivyo kutaka kuikosesha serikali mapato.

Kwa mujibu wa Aziz, ofisi ya mkuu wa wilaya hivi karibuni ilikaa na kamati ya ulinzi na usalama kwa lengo la kuhakikisha ulinzi kwenye maeneo ya mipaka kati ya Tanzania na Msumbiji unaimarishwa ili kudhibiti bidhaa mbalimbali za magendo zinazoingizwa nchini zinadhibitiwa kikamilifu.

Alisema katika kipindi cha masika, kwenye maeneo yote ya mipakani kumekuwa na tatizo la watu kuingiza bidhaa za magendo kutoka Msumbiji, yakiwamo mafuta ya kula.

Kuhusu mzigo uliokamatwa, alisema tayari umeshakabidhiwa ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wilayani Masasi kwa ajili ya taratibu za kisheria ambazo zinapaswa kufuatwa.

## DC apiga marufuku magunia ya lumbesa

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Singida, Pascas Muragiri, amepiga marufuku magunia yenye ujazo wa zaidi ya kilo 100 ya vitunguu vinavyouzwa na wakulima katika soko la kimataifa lililoko katika Manispaa ya Singida.

Muragiri alitoa amri hiyo alipokuwa akizungumza na wakulima na wafanyabiashara wa soko hilo alipofanya ziara ya kushtukiza kutokana na malalamiko kutoka kwa wakulima wa zao hilo.

Alisema mwaka uliopita, serikali ilipiga marufuku matumizi ya ujazo wa zaidi ya kilo 100 kwa gunia, maarufu kama 'lumbesa', ambayo wafanyabiashara wamekuwa wakitumia magunia ya nyavu yenye ujazo wa kilo 122. "Sasa vipimo tunavyovitumia kwenye kuuza bidhaa yoyote ile vipo kwa mujibu wa sheria na ukiangalia sheria sura namba 340 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 inatoa kipimo katika ujazo," alisema.

Mkuu wa wilaya alisisitiza kwamba kutokana na ukiukwaji huo wa sheria unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu na unaochangia kuwapunja wakulima, ni marufuku kwa wakulima kuwapunja wakulima na kwamba hatua kali zitachukulia kwa atakayekiuka agizo hilo. "Kwa tafsiri hiyo, kuanzia sasa ninavyozungumza vipimo vyote vyenye zaidi ya kilo 100 havitaruhusiwa kutumika katika wilaya nzima ya Singida. Iwe hapa sokoni au mashambani katika biashara hii ya vitunguu na yeyote atakayebainika ametumia gunia au neti yenye ujazo wa zaidi ya kilo 100 tutamchukulia hatua kali," alisema.

Muragiri pia alisisitiza kwamba kuanzia sasa wanaanza kufanya msako wa kuwatafuta wale wote wanaojaza zaidi ya kilo 100 kwa sababu alithibitisha mafanikio ya kazi hiyo yaliyopatikana katika viazi vitamu na mazao mengine.

Mwenyekiti wa Soko la Kimataifa la Vitunguu, Iddi Mwanja, alisema chanzo kikuu cha wafanyabiashara wanaonunua vitunguu kwa ujazo wa lumbesa ni Halmashauri ya Wilaya ya Singida na kutumia fursa hiyo.

Mwanja alimwomba mkuu huyo wa wilaya kuwakutanisha na uongozi huo ili kuwaelekeza namna ya kukusanya ushuru wao.

# Shirika la Italia laanzisha mafunzo kukabiliana mabadiliko tabia nchi

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

SHIRIKA la Istituto Oikos la nchini Italia linalofanya kazi nchini, limeanzisha kituo cha mafunzo kuhusu mabadiliko ya tabia nchi ili kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko hayo.

Kituo hicho kitakuwa katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) iliyopo nje kidogo ya Jiji la Arusha.

Uanzishwaji wa kituo hicho ni moja ya kampeni zinazofanywa na Oikos ili kuhamasisha jamii kuhusu mabadiliko ya tabia nchi kukabiliana nazo na kupunguza athari zake kwa jamii.

Kituo hicho kitakuwa na vituo vingine vidogo maeneo ya Oldonyowas, Oldonyosambu na Uwiro wilayani Arumeru.

Kwa upande wake, Meneja Mradi wa Eco Boma, Ifura Ukio, alisema kituo hicho cha kutoa elimu kitasaidia wakulima na wafugaji kupata uelewa kuhusu mabadiliko ya mfumo wa tabia nchi.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, mradi huo wa miaka minne unafadhiliwa kwa Umoja wa Ulaya (EU) chini ya Shirika la Dunia la Mabadiliko ya Tabia nchi (GCCA).

Kwa upande wa utekelezaji wa mradi huo nchini, umeanzisha ubunifu wa teknolojia 15 katika sekta tofauti kama vile za kilimo, nishati na misitu ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.



Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini mkoani Manyara, Pauline Gekul (wapili kushoto), akizungumza na wauguzi na madaktari wa hospitali ya mji huo baada ya kutembelea wodi ya wazazi juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Kalemani atoa siku tano Tanesco kufunga transfoma

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ametoa siku tano kwa Shirika la Umeme nchini (Tanesco), Mkoa wa Arusha, kufunga transfoma tatu eneo la Meru ili kuwawezesha wananchi wa eneo hilo kupata umeme mkubwa unaokidhi mahitaji yao.

Alitoa agizo hilo wakati wa ziara yake ya kutembelea kituo kikuu cha kupokea umeme wa gridi ya taifa, kilichopo Njiro jijini Arusha jana.

Dk. Kalemani alisema kumekuwa na malalamiko mengi ya wananchi wa eneo la Meru, wilayani Arumeru, kuwa wanapata umeme mdogo.

"Sasa nimeamua kuja kuangalia kituo hiki kinachopokea umeme kama upo wa kutosha, sasa nimejiridhisha upo umeme mwingi tatizo ni wafanyakazi wa Tanesco kupeleka transfoma za nyongeza tu, sasa nawapa siku tano mpeleke transfoma mbili au tatu eneo la Meru mkawafungie wapate umeme wa uhakika," alisisitiza.

Alisema umeme unapokuwa mdogo walalamikaji wengi hususani, wafanyabiashara ndio waathirika wakubwa na wapo wengi mkoani hapa.

Aliongeza kuwa baada ya kuongeza transfoma hizo hatategemea wafanyabiashara kulalamika tena na kupata visingizio vya kutolipa kodi, bali wautumie kuzalisha bidhaa nyingi katika viwanda vyao na bora, pamoja na kulipa kodi stahiki kwa serikali.

Pia aliagiza Tanesco ndani ya mwezi huu kuagiza kifaa maalum cha kukata umeme inapotokea hitilafu, mbili au na kuzihifadhi katika stoo ya kituo hicho kama akiba, ili inapoharibika mashine moja inachukuliwa ya akiba na kufunga mara moja.

"Mkiwa nazo za akiba mtaondokana na kuwaletea kero wananchi, ambao wanalalamika na ukosefu wa umeme pale inapotokea mashine imeharibika mnachukua siku nne kusubiri kije kifaa hicho baada ya kuagiza, sasa hakikisheni ndani ya mwezi huu mnanunua viwili au vitatu vya akiba ili mashine ikiharibika mara moja mnakiweka na wananchi wanaendelea kupata umeme," alisema.

Kwa upande mwingine aliagiza shirika hilo kuweka utaratibu wa kuwapa posho, walinzi wanaolinda miundombinu ya shirika katika kituo hicho usiku na mchana bila kupumzika, ili kuwapa moyo zaidi wa kufanya kazi hiyo bila kukata tamaa.

# DFID wakagua maendeleo mradi wa maji vijiji vitano

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAFADHILI wa mradi wa maji katika vijiji vitano vya Halmashauri ya Arusha, wilayani Arumeru, unaofadhiliwa na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa nchini Uingereza (DFID), wamekagua ujenzi wa utekelezaji wa mradi huo, unaotekelezwa na Shirika la Water Aid Tanzania kwa kushirikiana na halmashauri.

Mradi huo kwa sasa umefikia hatua ya tatu ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji baada ya hatua ya awali ya usanifu yakinifu wa uchimbaji wa kisima kukamilika katika shamba la Ilkiushini, Kitongoji cha Ekenywa, Kata ya Olturument.

Akizungumza katika ziara ya kukagua miundombinu ya mradi huo, Mtaalamu wa Mshauri wa Mradi wa Maji na Usafi kutoka DFID Tanzania, Lucas Kwezi, aliwataka makandarasi waliopewa zabuni ya ujenzi wa mradi huo, kuongeza kasi ya ujenzi ili kuukamilisha haraka na kwa wakati.

Aliwataka makandarasi hao, kwenda na muda waliokubaliana kwenye mikataba ya zabuni zao ifikapo mwishoni mwa Aprili, mwaka huu ili wakabidhi mradi ukiwa umekamilika.

Mhandisi Mkazi wa Shirika la WaterAid, Jailosi Chilewa, alisema hadi sasa utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 15, na matarajio yao utakamilika mwishoni mwa mwezi Aprili.

Alisema mradi huo umegawanywa katika mpangilio wa kazi katika sehemu kuu tatu, ambazo wametoa zabuni kwa kampuni tatu tofauti ambapo kampuni ya STS Construction Ltd, ujenzi wake utahusisha ujenzi wa miundombinu ya matangi ya kuhifadhia na kuchujia maji, usambazaji wa mabomba kwenye nyumba za watu pamoja na kusambaza mabomba kwenye vituo 20 vya kuchotea maji kutoka chanzo cha maji cha Emurtoto kuelekea Olkokola mpaka Lengijave kwa gharama ya Sh. bilioni 4.1.

Alisema kazi ya pili itatekelezwa na mkandarasi kutoka Kampuni ya Advance Ltd kwa kushirikiana na Meero Contractors Ltd, na watajenga nyumba za kusukuma maji, matangi mawili ya kukusanyia maji, tangi moja la kuhifadhia maji, nyumba ya kuhifadhia mitambo ya kutibu maji, kusambaza mabomba kutoka chanzo cha maji Ilkiushini mpaka tangi la kuhifadhi maji la Leomoja kwenda Lengijave kwa gharama ya Sh. bilioni 1.7.

Hata hivyo, kazi ya tatu itafanywa na mkandarasi kutoka Kampuni ya ASES Ltd, ambao watajenga matangi mawili ya kuhifadhi maji, watasambaza mabomba umbali wa kilomita 34, kutoka Leomoja kwenda tangi la Ngaramtoni na kujenga vituo 46, vya kuchotea maji kwa gharama ya Sh. milioni 937.

Aidha, wataalamu wa ujenzi wa mradi huo, wamewaomba wananchi wanaoishi maeneo ya mradi unapotekelezwa washirikiane na makandarasi kulinda vifaa vinavyoletwa kwa ajili ya kujenga miundombinu hiyo.

# Mawaziri walivyosota saa 11 kusaka suluhu mgogoro wa mwekezaji

**Na Godfrey Mushi,** HAI

HATIMAYE mawaziri wawili wamehitimisha kikao cha kutafuta ufumbuzi wa mgogoro wa wawekezaji katika Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, huku serikali ya Mkoa wa Kilimanjaro na wana ushirika wakitaka kuitwa mwekezaji aliyopo nje ya nchi.

Kikao cha mawaziri hao kilitumia dakika 660 sawa na saa 11 kwa ajili ya kujadili kwa kina ili kubaini ushahidi kwa lengo la kushughulikia malalamiko ya wawekezaji katika wilaya hiyo ili kuhitimisha mgogoro huo.

Waziri wa Fedha, Dk. Philip Mpango na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia uwekezaji, Angela Kairuki, wameafiki kuitwa kwa mwekezaji wa awali wa Kampuni ya Tudeley Estates Ltd, Conrad Leg ambaye aliingia mkataba na vyama vinne vya ushirika vinavyounda ushirika wa Murososango.

Akizungumza baada ya kumalizika kikao hicho kilichofanyika juzi kuanzia saa 3:00 asubuhi na kumalizika saa 1:28 usiku, Waziri wa Fedha, Dk. Mpango, alisema katika kikao hicho wamezungumza na wananchi ambao ni wana ushirika wa mashamba ya Kibo na Kikavu na wao wamewaeleza kuwa wao ndio waliingia mkataba wa kwanza na mwekezaji wa kwanza wa Kampuni ya Tudeley Estates Ltd ambaye Mkurugenzi wake anaitwa Conrad Leg.

"Kwa hiyo wametueleza changamoto walizokuwa nazo kwamba mtu ambaye waliingia naye mkataba alifika mahali akaondoka, wakaja hawa wengine ambao ni pamoja na hawa wa kutoka Ujerumani, wanasema wanataka kununua zile hisa za yule bwana aliyeondoka, lakini mkataba wa awali ulikuwa haujaisha, kwa hiyo hawa wana ushirika wakasema itakuwaje? Lazima arudi yule wa kwanza tumalizane kwanza, tujue kama ni kuvunja mkataba, tujue mkataba umevunjika.

"Hatuwezi kuingia mkataba na mtu mwingine tena, itatuletea migogoro, lakini wakati huo huo huyu mwekezaji wa pili tayari akawa ameshaingia na analeta fedha kutoka kwenye kampuni nyingine analipa madeni ya ile kampuni ya kwanza ni fedha nyingi amewekeza, amelipa baadhi ya kodi, akalipa baadhi ya madeni, lakini pia miundo mbinu ya pale shambani.

"Kwa hiyo akawa anasema na sisi tunahaki, akiulizwa sasa una haki ipi kwa mikataba ipi, tatizo. Anasema wale wenzangu wale, yule tuliyekuwa tunataka kuingia naye mkataba ameingia mitini."

Waziri Mpango alisisitiza, wamekubaliana ni muhimu mwekezaji wa kwanza aliyeingia mkataba na Muungano wa Vyama vya Murososango akapatikana ili kuondoa mambo yasiyoeleweka.

"Tunataka tuje tuondoe haya mambo yasiyoeleweka na kumaliza ule mkataba wa kwanza, halafu tuone hawa wengine wanaweza wakaingia mkataba gani, lakini uwe ni mkataba ambao unawanufaisha wananchi wenye yale mashamba. Ndio msisitizo wetu. Hatuwezi kuingia mikataba ambayo wananchi wetu na hasa wale wa chini wanaishia kunyanyasika na hata hizo hisa walizokuwa nazo hawajapata chochote," ameeleza Waziri Mpango.

Kwa mujibu wa Waziri Mpango, kikao hicho kiliitishwa ili kuwasikiliza wadau wote, lakini akakiri kwamba yako mambo ya kisheria ambayo bado yanahitaji kufanyiwa kazi na tayari wameomba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iweze kutazama baadhi ya mambo ya kisheria na kuwashauri ili wasije wakafanya maamuzi ambayo yanaweza yakaiingiza serikali hasara.

Kwa upande wake, Waziri Kairuki ameeleza wazi kwamba walianza kazi hiyo wiki mbili zilizopita katika Wilaya ya Rungwe (Mbeya), kwa sababu kuna jambo ambalo limemhusisha mwekezaji ambaye amewekeza Rungwe, lakini pia mwekezaji huyo huyo, kuna suala limejitokeza katika Wilaya ya Hai.

Waziri huyo wa uwekezaji, amesema katika Wilaya ya Hai zipo kampuni mbili, kampuni moja inaitwa Tudeley Estates Limited na kampuni ya pili inaitwa Kuza Afrika lakini hapo hapo pia kuna Kibo Plantation na Kilimanjaro.

Amesema wawekezaji, baadaye walienda mbali zaidi na kuwekeza katika kilimo cha maparachichi kama ambavyo inafanyika katika Wilaya ya Rungwe, lakini katika uwekezaji huo kwa sehemu moja inaonekana waliingia mikataba mingine pamoja na hiyo ya Kampuni ya Kuza Afrika ambayo ilikuwa wameingia kwenye suala la mauziano na kuwekeza katika eneo hilo la vyama vya ushirika.

"Kuna changamoto, wakati huo huo kuna masuala ya kikodi, kuna akaunti za mwekezaji zimefungiwa, tukaona ni vyema tuje hapa tuweze kutatua changamoto ili vyama vya ushirika vielewe, mwekezaji yupi ambaye wameingia naye mkataba na yupi ambaye watashirikiana naye katika suala zima la uwekezaji wa kilimo katika wilaya hii ya Hai," amesisitiza Kairuki.

Amesema katika kikao chao hicho walikuwa wakiangalia suala zima la michakato ilivyofanyika, kama mchakato na taratibu za kufunga akaunti ilikuwa sahihi au laa, lakini nini kinapaswa kufanyika ili mwekezaji awe sawa pia na serikali nayo iweze kupata mapato yake.

Waziri Kairuki ameeleza kwamba ujio wao ni mahususi kwa ajili ya kupata ushahidi, kuweza kupata namna ambavyo taratibu mbalimbali za uwekezaji zilifanyika lakini pia kuweza kuona kwamba wao wenyewe vyama vya ushirika wanataka nini.

"Tulikuwa tunaangalia kwamba, je, wanataka kuendelea na uwekezaji? Je, wanataka kuendelea na mwekezaji huyu ambaye yuko sasa, au wanataka kitu gani? Lakini pia kuweza kusikia kutoka kwenye serikali ya mkoa na serikali ya wilaya na wenyewe wanawaonaje wawekezaji hao ambao wapo. Je, wanaona maslahi ya taifa yanalindwa au laa?

Lakini pia masuala ya ulipaji wa kodi na mambo mengine kwa namna gani yanatimizwa kikamilifu," ameeleza Kairuki.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, akizungumzia sakata hilo amesisitiza, tumekutana hasa kwa ajili ya uwekezaji wa shamba kubwa la kahawa, kuna mgogoro wa muda mrefu na tumefikia mwafaka mzuri.

"Mwekezaji wa awali wa Tudeley Estates Ltd, jina lake anaitwa Conrad Leg na ndiye aliyeingia mkataba na vyama vinne vya ushirika wilaya ya Hai ambavyo kwa pamoja vinajiita Murososango. Lakini vijiji vyote viko Masama, ndio maana inaitwa Kibo/Kikavu ambayo yote ni takribani ekari 2054 kwa ujumla," amefafanua Dk. Mghwira.

Pamoja na mambo mengine, Mkuu huyo wa Mkoa ameelezea kwamba katika kikao hicho wamekubaliana wote kwa pamoja kwamba huyo mwekezaji wa awali aliyeingia mkataba na vile vyama vya ushirika aitwe kwa sababu akija yeye hayo mambo mengine yote yatamalizika.

"Suluhu kubwa kabisa ni yeye kufika na kutupa fursa sasa ya kusikilizana wadau wote ili tumalize hili jambo kwa lengo la kundelea na uzalishaji uendelee, mpaka sasa shamba linafanya kazi robo tu, kwa hiyo hii sehemu imekaa bure kwa sababu ya migogoro ambayo tunaweza kuimaliza mapema.



Waziri wa Fedha, Dk. Philip Mpango (aliyesimama) akifafanua jambo kabla ya kuanza kwa kikao hicho cha kushughulikia wawekezaji katika Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA:GODFREY MUSHI**

ama
ALHAMISI MACHI 7, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 19

**Mlo kamili kwa mwenye VVU**



Ukurasa 16

Wanawake walivyotumia mlango Tasaf kuibua mradi maji Kibaha



Ukurasa 14

**Vijue vyanzo na hali ya vifo duniani**



## SIKU YA USIKIVU DUNIANI

# Ummy Mwalimu: Haya maisha ya 'foni' nasi tumekaa pabaya

Ukurasa 15

# Vijue vyanzo na hali ya vifo duniani

TAKWIMU za mwaka juzi zinaonyesha kuwa watu milioni 56 walikufa. Hata hivyo, inaelezwa idadi ya watu inaongezeka, pia wastani wao wa kuishi

Katika vifo hivyo, takwimu zinaonyesha zaidi ya asilimia 10 ya vifo hivyo, chanzo chake ni magonjwa yasioambukiza na ya muda mrefu.

Ugonjwa ambao unaua watu wengi ni shambulio la moyo ambao unaathiri moyo na mishipa.

Idadi ya vifo vinavyosababishwa na mshtuko wa moyo viko juu mara mbili ya vyanzo vya saratani, ugonjwa ambao wa pili kusababisha vifo duniani.

Inaelezwa wastani uliopo ni kwamba, katika kila vifo sita, kimoja kinakuwa kinasababishwa na saratani.

Magonjwa mengine vinara yanatajwa kuwa ni kisukari, magonjwa yanayoadhiri mfumo wa kupumua na maradhi ya akili.

Hata hivyo, kuna angalizo kutoka watafiti wa kimataifa na Shirikla la Afya Duniani (WHO) kwamba, watu wengi wanakufa kwa magonjwa yanayozulika.

Takribani, watu milioni 1.6 walikufa kutokana na ugonjwa wa kuhara mwaka 2017, hali inayouweka ugonjwa huo kuwa miongoni mwa sababu 10 za vifo.

Pia, magonjwa ya ulemavu wa watoto unaosababisha vifo vya watoto chini ya siku 28 ni sababu ya vifo milioni 1.8 mwaka kwa 2017. Idadi na vyanzo vya vifo vinatofautiana baina ya nchi na nyingine. **BBC**



Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dk. Tedros Adhanom Ghebreyesus. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

## SIKU YA USIKIVU DUNIANI

# WHO: Vijana bilioni watumia 'foni' hatarini kupata uziwi

SIKU ya Kusikia Duniani, kila mwaka ni Machi 3. Wakati maadhimisho hayo yakiendelea, kuna jumla ya vijana zaidi ya bilioni moja wenye umri kati ya miaka 12 na 35 wanaelezwa kujiweka katika hatari ya kupata uziwi usioweza kutibika, kwa sababu ya kusikiliza sauti za juu za vitu kama muziki, kwa kutumia simu za kisasa zinazoweza kufanya mambo mengi.

Hivi karibuni, wataalamu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), walitoa angalizo katika uzinduzi wa mwongozo mpya unaosaidia kushughulikia tatizo hilo.

Mapendekezo yaliyotolewa katika mwongozo huo, ni kupunguza tatizo la watu wengi kupata uziwi kwa kusikiliza sauti za juu. Hapo inajumuishwa utendaji mzuri wa vifaa vya kusikilizia vinavyoweza kudhibiti uwiano wa sauti, ikiwa ni ya juu sana, muda ambao watu wanasikiliza muziki kutumia vifaa hivyo.

Mtaalamu wa kiufundi wa WHO anayehusika na masuala ya kuzuia uziwi na kupoteza uwezo wa masikio kusikia wa WHO, Dk. Shelly Chadha anasema:

"Vijana zaidi ya bilioni moja wako hatarini kupata uziwi kwa sababu tu ya kufanya kile wanachokifurahia zaidi kila mara, ambacho ni kusikiliza muziki kupitia vipokea sauti vinavyobanwa kichwani (headphones)".

Anaongeza: "Kwa wakati huu, hatuna kitu chochote kinachoshikika, isipokuwa ni hisia zetu tu zikituambia 'unachofanya ni sahihi au je hiki ni kitu ambacho kitatusababishia kupoteza uwezo wetu wa kusikia au uziwi katika miaka michache ijayo?"

Mradi wa pamoja wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) na Muungano wa Kimataifa wa Mawasiliano (ITU), ni jaribio la kutaka kukabiliana na tatizo la kutokuwa na ufahamu, kuhusu athari za kusikiliza kelele kubwa, wakati kukiwapo takwimu zinazoonyesha kwamba, takriban asilimia 50 ya vijana wanasikiliza sauti katika viwango visivyo salama.



Daktari akimhudumia mgonjwa wa masikio. Picha ndogo; simu na vifaa vya kusikilizia ambavyo vimekuwa chanzo kikubwa cha matatizo ya usikivu duniani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **"Ikizingatiwa ujuzi upo na teknolojia tunayo ya kuzuia uziwi, ni kwa nini vijana waendelee kuharibu ngoma zao za masikio wakati wakisikiliza muziki.**



Hiyo ni kupitia vifaa binafsi, zikiwamo simu za kisasa ambazo matumizi yake yanaendelea kuongezeka duniani.

Kwa WHO, hivi sasa hili tatizo la kupoteza uwezo wa kusikia, ambalo halijashughulikiwa, inaugharimu uchumi wa dunia dola milioni 750.

### MAPENDEKEZO GANI?

Dk. Chadha anasema: "Inabidi kufikiria kwamba suala hili ni kama kuendesha gari kwenye barabara kuu, lakini bila kuwa na kidhibiti mwendo.

"Tulichokipendekeza ni kwamba simu za kisasa za rununu zije zimewekwa vifaa vya kudhibiti sauti ambavyo vitakuwa vinakuelezea ni kiwango gani cha sauti unakipata na kukujulisha endapo kimependukia au la."

Chaguo la wazazi kudhibiti sauti pia lijumuishwe. Mapendekezo haya yamejumuishwa pia kwenye mapendekezo ya Umoja wa Mataifa kwa sekta husika, ambayo ilishiriki katika miaka miwili ya majadiliano na wataalamu wa serikalini, vyombo vinavyohusika na wanunuzi na asasi za kiraia.

Mwongozo huo mpya unapendekeza kutumia teknolojia, ili kuandaa wasifu wa wasilikilizaji kwa kufuatilia ni kwa kiasi gani wanatumia vipokea sauti vinavyobanwa kichwani, kisha kuwajulisha kama matumizi yao ni salama au la.

Pia, Dk. Chadha anaieleza teknolojia hiyo kuwa: "Ni ile ya kudhibiti moja kwa moja au kupunguza sauti bila mtumiaji kufanya hivyo ili wakati ambapo mtumiaji anazidi kiwango cha sauti inayostahili kifaa hicho kinapunguza chenyewe ili asiathiri masikio yake."

Kwa mujibu wa WHO, zaidi ya mtu mmoja kati ya 20 miongoni mwa watu wazima milioni 432 na watoto milioni 34, wana matatizo ya kupoteza uwezo wa kusikia au uziwi, unaoathiri maisha yao.

Utafiti wa WHO umebaini kwamba, waathirika wengi wanaishi katika nchi masikini au za kipato cha wastani, na kwamba ifikapo mwaka 2050 zaidi ya watu bilioni 900 watakuwa na matatizo ya uwezo wa masikio kusikia.

Dk. Tedros Gebreyasus, ni Mkurugenzi Mkuu wa WHO, anayesema takriban nusu ya mikasa yote inaepukika, kwa kuchukua hatua za kudhibiti afya ya jamii.

Anasisitiza kuwa: "Ikizingatiwa ujuzi upo na teknolojia tunayo ya kuzuia uziwi, ni kwa nini vijana waendelee kuharibu ngoma zao za masikio wakati wakisikiliza muziki. Ni lazima waelewe kwamba pindi watakapopata uziwi basi hawawezi kusikia tena". UN

• *Soma zaidi Uk 15*

AFYA

SIKU YA USIKIVU DUNIANI

# Ummy Mwalimu: Haya maisha ya 'foni' nasi tumekaa pabaya

**Na Yasmine Protace**



Huduma ya ukaguzi na tiba ya masikio ikifanyika nchini. **PICHA: MAKTABA.**

KAMA lilivyotamka Shirika la Afya Duniani (WHO), matumizi ya spika za masikioni, maarufu kama 'headphones' au wengine huiita 'foni' sasa madhara yameshaanza kujitokeza, inachangia usikivu hafifu kwa umma.

Hiyo inashuhudiwa sasa kwa madereva wa magari na bodaboda ambapo imekuwa sehemu kuu ya maisha yao.

Katika usafiri wa umma, kama vile daladala ni kawaida kushuhudia vijana wameshika simu huku wakiwa na spika masikioni.

Pia, ndiyo kawaida ya vijana wanaotembea, muda wote wanasikiliza kupitia spika za masikioni. Ni ishara tosha namna watu wanavyoharibiwa na uhalisia huo.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili- Mloganzila jijini Dar ss Salaam, katika kuadhimisha Siku ya Usikivu Duniani, anakiri hilo ya uharibifu wa kiafya.

Waziri Ummy, anasema kuwa matumizi ya simu za kisasa yameongeza kasi ya watu kutumia spika za masikioni, linalohatarisha watu wengi kuwa na matatizo ya usikivu.

"Unakuta kijana kuanzia asubuhi mpaka jioni, ameweka spika za masikioni. Anasikiliza muziki, hawajui wanajiweka katika hatari ya kupata tatizo la usikivu" anasema Waziri Ummy na kudokeza kwamba, kundi hilo la vijana liko hatarini katika matatizo ya usikivu.

Waziri Ummy anatumia nafasi hiyo kutoa rai kwa wananchi kupunguza matumizi ya spika za masikioni, ili kuweza kujikinga na matatizo ya usikivu.

"Nitoe rai kwa vijana wapunguze matumizi ya spika za masikioni kwa muda mrefu, tusipo kuwa makini tunaweza kujikuta tuna taifa lenye watu wengi wenye matatizo ya kutosikia vizuri," anasema Waziri Ummy.

### VYANZO VINGINE

Waziri Ummy anaesema tatizo la usikivu hutokea kwa njia mbalimbali, ikiwemo baadhi ni ya kuzaliwa na wapo wanaolipata ukubwani kutokana na sababu tofauti.

Anaainisha sababu hizo ni pamoja na kukaa kwa kwa muda mrefu kwenye sehemu zenye kelele nyingi na matatizo yanayoambata na afya ya sikio.

Waziri Ummy, anasema kuwa jambo jema ni kuona sasa matibabu ya matatizo ya usikivu hafifu yanapatikana hapa nchini na rai yake ni kuwataka wananchi kukata bima za afya, ili wapate matibabu ya uhakika.

> "Nitoe rai kwa vijana wapunguze matumizi ya spika za masikioni kwa muda mrefu, tusipo kuwa makini tunaweza kujikuta tuna taifa lenye watu wengi wenye matatizo ya kutosikia vizuri.

"Serikali imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha tatizo hili linazuiliwa kabla ya kutokea, pia, kuhakikisha matibabu yanapatikana yakiwemo kutumia mashine ya mawimbi ya sauti, upasuaji wa kuziba tundu la ngoma ya sikio pamoja na kupandikizwa vifaa vya kusaidia kusikia" anasema Waziri Ummy.

Hata hivyo, anasema takwimu zinaonyesha kuwa mwaka 2018 Hospitali ya Taifa Muhimbili imefanikwa kuwapatia wagonjwa 116 vifaa vya mawimbi ya sauti, wagonwja 43 walifanyiwa upasuaji wa kuziba tundu la ngoma ya sikio.

Anaongeza kuwa serikali itaendelea kuboresha huduma za matibabu ya kibingwa na kuhakikisha matibabu yanapatikana nchini.

### MKURUGENZI MUHIMBILI

Awali akitoa taarifa yake, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Makwaiya Makani, anasema wamekuwa wakifanya jitihada mbalimbali katika eneo la usikivu, ikiwemo huduma ya upandikizaji vifaa vya usikivu kwa watoto wenye matatizo ya hayo.

"Tangu mwezi Juni mwaka 2017, tayari watoto 21 wamepandikizwa vifaa vya usikivu kitaalamu kwa jina la 'cochlear implants" anasema Makani



Kifaa cha usikivu wa simu chenye madhara sikioni.

Makani anaesema kuwa wameendesha kliniki ya siku mbili katika Hospitali ya Mloganzila, kutoa huduma za uchunguzi na matibabu ya matatizo ya usikivu, ambayo watu 264 wamejitokeza na kati yao watu 172 walihitaji uchunguzi zaidi wa usikivu.

Pia, anaeleza watu 64 walikutwa na matatizo ya usikivu na tayari wameshapatiwa rufaa kwa ajili ya matibabu zaidi na watu 31 wamekutwa na nta za masikioni.

Dk. Makwaia anasema, kuna watu 26 waliokutwa na maambukizi kwenye masikio, ambao wamepatiwa rufani ya matibabu zaidi. Tatizo la usikivu, linaelezwa kwamba linazidi kuongezeka kila siku na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia tano ya watu duniani wana tatizo la usikivu.

Anasema, tatizo hili litaongezeka maradufu kila mwaka. Inatakiwa kila mmoja achukue hatua kujikinga na tatizo hilo, ikiwemo kuepuka sehemu zenye kelele, pia kusikiliza muziki kwa sauti kubwa na muda mrefu, kwa kutumia spika za masikioni.

MAZINGIRA

# Wanawake walivyotumia mlango Tasaf kuibua mradi maji Kibaha

• Kwenye ukame, sasa maji yako kibao



Na Elizabeth Zaya

MAUA Salehe ni mwanakijiji wa kijiji cha Vikuge Kitongoji cha Ngoingo kilichopo wilayani Kibaha, mkoa wa Pwani.

Yeye ni mnufaika wa mpango wa Uhawilishaji fedha kwa kaya masikini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), anayesimulia namna ambavyo mpango huo umewasaidia hasa kupitia miradi mbalimbali, ambayo wameanzishiwa na mfuko huo.

Maua anasimulia kwamba wamekuwa wakipewa ruzuku kwa kaya katika mpango, pia wakipatiwa elimu ya kuwasaidia kuanzisha na kuendesha miradi, ikiwamo kilimo, ufugaji samaki kupitia mabwawa ya kutengeneza na shughuli za mtu mmoja mmoja.

Maua anasimulia namna walivyoondokana na tatizo la maji, kupitia miradi ya uchimbaji mabwawa na visima, baada ya kuunganisha nguvu ya pamoja kwa walengwa wote wa mpango, kwa kutumia elimu ya ujasiriamali waliopewa.

"Tuliteseka kwa miaka mingi hapa kijijini kwetu, kwa tatizo la maji. Miaka yote tumekuwa tukifuata maji mbali. Mwaka jana, Tasaf walituambia tupendekeze miradi ambayo tunaona inaweza kutusaidia na mawazo ya haraka tuliyopata ni mradi wa maji," anasema.

"Kwa hiyo, ilibidi mkutano uitishwe kwa walengwa wote ambapo tuliambiwa kwamba tunatakiwa kujipanga kuanza uchimbaji wa visima.



Kinamama wa Vikuge, Kibaha wakisafisha bwawa walilotengeneza, ukiwa ni mradi unaotokana na ufadhili wa Tasaf. Picha ya juu ni sehemu ya bwawa hilo ambalo sasa ni chanzo cha maji katika eneo hilo lililokuwa kame. **PICHA ZOTE: ELIZABETH ZAYA .**

"Baada ya kupata wazo hilo na kuwaambia wataalam, walianza kufanya utafiti wa kutafuta eneo linaloweza kufaa kwa ajili ya kuchimba visima na walifanikiwa kupata eneo ambalo nalo walisema maji yake yako mbali, japo walisema ndilo lilikuwa nafuu.

"Kwa hiyo, ilibidi mkutano uitishwe kwa walengwa wote ambapo tuliambiwa kwamba tunatakiwa kujipanga kuanza uchimbaji wa visima," anaongeza Maua.

Anasema, eneo lilikuwa na magugu mengi, lakini kwa sababu wataalam walisema linaweza kupatikana maji, walianza kulisafisha kwa ajili ya kuanza uchimbaji, japo wengi wao hawakuamini kama maji yangepatikana.

"Lilikuwa ni eneo lenye magugu mengi na lilikuwa na majani marefu. Siku ya kwanza kuanza, kuchimba ilibidi tuyaondoe yote na kuanza kukwatua.

"Tulianza kuchimba wote si wanawake wala wanaume na kutokana na maelekezo ya wataalamu, walishauri kwamba tungeweza kuchimba hata bwawa kwa hiyo ilibidi tukazane ili tupate bwawa," anafafanua Maua

Mwanakijiji huyo anasema, walikuwapo walengwa zaidi ya 100, lakini kazi ya uchimbaji iliwachukua siku mbili na ya tatu asubuhi ndiyo iliisha.

"Haikuwa kazi rahisi, lakini tulijituma mpaka tukafanikiwa. Tulisomba udongo wote kwa kutumia ndoo zetu. Wanaume walikuwa nje na wanawake tukawa ndani ya shimo kuchota udongo wote.

"Kwa kutumia ndoo zetu na kubeba kichwani na wanaume wanachukua na kutupa nje, japokuwa baada ya kumaliza maji hayakuwa mengi, lakini kadri siku zilivyosogea, maji nayo yalikuwa yanaongezeka," anasimulia.

### VISIMA VIPYA

Anasema, walipomaliza kuchimba bwawa, walianza kazi ya kuchimba visima kuzunguka eneo hilo la bwawa ambalo lengo lilikuwa kwa ajili ya maji ya kutumia majumbani, huku wakiliwekea malengo ya kufugia samaki.

"Kwa kweli hatukuamini kama tungefanikiwa. Hata, wakati yule mtaalamu anatuambia kwamba ingewezekana, hatukumwamini.

"Tulikuwa tunamwitikia tu ili tusimkatishe tamaa, kwa sababu miaka yote tumeishi hapa na hatujawahi kusikia kitu kama hicho na taabu ya maji imekuwa ya muda mrefu," anaeleza Maua.

Anaeleza kwamba, wiki moja baada ya kuchimba bwawa na visima hivyo, maji yalianza kujaa, huku katika bwawa hayakujaa, lakini waliendelea kusafisha kwa siku kadhaa mpaka yalipoanza kujaa katika bwawa hilo, huku wakianza kutumia kuoga na kufulia maji ya visima.

"Bahati nzuri tulichimba kipindi cha msimu wa mvua. Kwa hiyo, tulibahatika kukaa kwa muda mfupi, mvua nayo ikanyesha, ikaongeza maji kwenye bwawa. Kwa hiyo, ikawa imesaidia na kadri tulivyoendelea kusafisha maji yalizidi kuwa mengi na masafi," anasema Maua.

"Yaani, kwa kweli kwa sasa kama unavyotuona. Hivi ndivyo kilio chetu cha shida ya maji katika kijiji hiki kilivyoisha, sasa hivi imebaki kama historia.

"Sisi wanufaika wa Tasaf tunanufaika na maji, lakini pia tumewasaidia wananchi wote wanaoishi katika kijiji hiki kutumia maji haya ya visima vyetu," anaeleza.

Maua anasema uwapo wa maji mengi katika bwawa hilo, kunasaidia hata maji katika visima vya pembezoni yasikauke.

"Kuna wakati maji yalikuwa yakipungua katika bwawa, pia ilikuwa inaathiri hadi huku kwenye visima. Lakini, ni muda sasa tangu itokee hali hiyo, hatujashuhudia tena bwawa likipungua na kwa maana hiyo, hata visima vyetu havijapungua maji na tunatumia sana.

"Kwa kweli tunaishukuru sana Tasaf kwa kutuletea wataalam wa kutusaidia kugundua hili na kutuletea vifaa vya kuchimbia maana bila wao mpaka sasa tungekuwa tunapata shida," anasema Maua.

Anasema, tayari wameanza kufuga samaki katika bwawa hilo na kwamba lengo ni kuhakikisha linazalisha samaki wa kutosha, kwa ajili ya kunufaisha walengwa wote wa mradi wa asasi hiyo.

"Sisi wanufaika wa Tasaf tunanufaika na maji, lakini pia tumewasaidia wananchi wote wanaoishi katika kijiji hiki kutumia maji haya ya visima vyetu.

"Tunatarajia kwamba, samaki wakizaliana wengi tutapata chakula na tutauza kujiongezea kipato, kwa miradi hii tunayoanzishiwa na Tasaf. Kwa kweli umasikini kwa heri, tunaishukuru sana pamoja na serikali yake," anasema.

### MTAALAM VISIMA

Juma Ibrahim, ni mtaalam visima, ambaye ni msimamizi wa miradi ya nguvukazi ya walengwa hao, aliyegundua bwawa hilo, anasema wanatarajia kwamba baada ya mwaka mmoja, samaki katika bwawa hilo watakuwa tayari kwa ajili ya chakula.

"Tunachofanya hivi sasa ni kuwapa ushauri hawa walengwa, namna bora ya kulitunza ikiwamo kulifanyia usafi na mambo mengine ya kusaidia, kulinda samaki waendelee kuzaliana na wasipate athari zozote," anasema Ibrahim.

Anasema, katika kijiji hicho wana mabwawa mawili ya walengwa na yote yalipatikana kwa mtindo huo wa kuchimba na kwamba yote wanafuga samaki.

"Na lengo ni kuwapatia elimu kuhakikisha wanaanzisha miradi mingi iwezekanavyo kwa ajili ya kuinua kipato chao," anasema Ibrahim.

Mbali na mradi huo, anasema walengwa wa kijiji hicho, pia wanaelimishwa uanzishaji shughuli zao nyingine za kujiingizia kipato, ikiwamo kilimo cha mtu mmoja na vikundi na tayari wanalima mihogo.

Anasema shamba hilo la mihogo, ni la walengwa wote na wanalitumia kama shamba darasa, kwa ajili ya kuwasaidia kulima kisasa katika mashamba yao mengine.

## Mama anaweza kubeba mimba kabla mwaka tangu ajifungue

WAKATI kinamama wamezuiwa kiafya wasubiri walau uishe mwaka ndipo abebe mimba nyingine tangu ajifungue, kuna ushahidi kwamba mambo yamebadilika, mama anaweza kuzaa muda huo.



Mama akimnyonyesha mtoto wake. **PICHA: MTANDAO.**

Katika utafiti wa kimataifa uliohusisha watu 14,000 imedhihirisha uhalisia na sasa kuna imani mama anaweza kuzaa katika muda huo wa mapema, chini ya mwaka mmoja.

Nchini Uingereza kulikofanyika utafiti huo na kushirikisha nchi nyinginezo, rekodi iliyopo ni kwamba, wastani wa mtoto mmoja kati ya 225 wanaozaliwa, hufa ndani ya umri wa wiki 25 ambayo ina wastani wa miezi sita.

Hata hivyo, maono hayo ya kitafiti yanaonyesha kuwa, tangu mwaka 2000, kasi ya vifo hivyo kwa upande wa Uingereza sasa inaanza kupungua.

Katika kila nchi, kuna utaratibu wake wa kusimamia uzazi wa mpango, huku katika ngazi ya juu kukiwapo miongozo chini ya Shirika la Afya Duniani (WHO).

Mtaaluma wa Chuo Kikuu cha Manchester, Profesa Alex Heazell, anasema kwao wataalamu, hawana shaka kwamba watafanikiwa katika hilo.

"Ili mradi wanapata taarifa zote kuhusu kwanini watoto wao hufa, chaguo la lini kuwa na mtoto liko katika mitazamo yao (kinamama)," anasema Profesa Heazell.

Ni utafiti uliofika mbali katika nchi za Australia, Finland na Norway, ikifanya tathmini inayofuatilia rekodi za jumla ya miaka 37 ikionyesha mafanikio makubwa.

Matokeo ya utafiti huo, ulioongozwa na Dk. Annette Regan, wa Chuo Kikuu cha Curtin, nchini Australia, anaeleza matokeo hayo ni ya tija kwa matumizi ya huduma za kliniki za uzazi katika nchi mbalimbali duniani.

Hata hivyo, anagusia hoja ya kinamama kuwa makini kuhakikisha kabla hajapata mimba nyingine, anahitaji kuiachia muda wa kutosha afya yake ili iboreke, kwani inaweka mbali na matukio kama mimba kutoka.

Akitoa maoni yake kuhusu utafiti huo, mtaalamu bingwa Mark A Klebanoff, kutoka taasisi ya utafiti katika hospitali iitwayo Nationwide Children's Hospital ya Marekani, anasema pamoja na mafanikio hayo, kuna mambo ya kutiliwa maanani.

Anataja baadhi ni hali halisi ya mwanamke mhusika kabla ya kupata mimba, umri wake, ukubwa wa famili aliyonayo na hisi binfasi ya haja ya kuwa na mimba tena. **BBC.**

AFYA

# Mlo kamili kwa mwenye VVU

**Na Barnabas Maro**

• Simulizi ya umeng'enyaji, mtindi, kitunguu



Mtoto akilishwa. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

KUTOKANA na dai la lishe bora kwa wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU), jamii imekuwa ikitafuta habari na elimu inayohusu uhusiano kati ya lishe bora na Ukimwi.

Mtaalamu, Dk. G.D Ndossi, anasema wahitaji hao hawapati majibu sahihi, kulingana na wanayohoji. Taasisi ya Chakula na Lishe, kupitia kitabu chake, imeandaa mwongozo kuwasaidia wahusika, kama wahudumu afya na huduma za majumbani.

**MLO KAMILI NINI?**

Maana yake ni mchanganyiko wa vyakula vya makundi, yenye virutubishi muhimu na kutosheleza afya bora. Hiyo inajumuisha nafaka, mizizi na ndizi za kupika.

Katika fungu hilo, kunapatikana mahindi, ulezi, mtama, uwele, mchele, ngano, viazi vikuu, viazi vitamu, muhogo, magimbi na ndizi za kupika.

Pia, kuna kunde, maharage, choroko, njegere, mbaazi, njugumawe, dagaa, samaki, nyama, maini, figo, jibini, maziwa, mayai, senene na kumbikumbi.

Kundi la mboga linajumuisha mchicha, tembele, majani ya maboga, majani ya kunde, kisamvu, mnafu, bamia, karoti, pilipili mboga (pilipili hoho), nyanya, mlenda, mchunga, figili, sukuma wiki, biringanya na spinachi.

Matunda yana:Maembe, pera, papai, chenza, nanasi, ubuyu, bungo, ukwaju, chungwa, fenesi, topetope, stafeli, pasheni na peasi.

Aina nyingine ya mlo inajumuisha mafuta, sukari na asali, hasa mafuta yatokanayo na wanyama kama samli, siagi, mafuta ya samaki na magarini.

Mafuta ya mimea yapo yatokanayo na nazi, alizeti, karanga, pamba, mawese, sukari guru, miwa na asali.

Katika mlo, mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano, anatakiwa kupata milo mitano kwa siku; mtu mzima, si chini ya milo mitatu na mjamzito au mama anayenyonyesha, anahitaji zaidi ya milo mitatu, kukidhi mahitaji makubwa aliyo nayo.

**MASWALI & MAJIBU**

**Swali: Watu wanashauriwa kutumia matunda katika mlo wao. Je, iwe kabla, wakati anakula au baada ya hapo?**

**Jibu:** Matunda yanaliwa wakati wowote, ila ni vizuri wakati wa chakula kusaidia ufyonzwaji wa virutubishi muhimu vilivyoko kwenye chakula.

Kwa mfano, matunda yana vitamin C husaidia ufyonzaji madini ya chuma kutoka kwenye chakula.

Pia, Vitamini A inapatikana kwenye matunda, lakini haifyonzwi vizuri tumboni, mpaka yachanganyike na mafuta. Ni vizuri matunda yaliwe na chakula, ili mafuta yaliyoko kwenye chakula, yasaidie ufyonzwaji wa vitamini hiyo.

> **"Asilimia 75 ya mahitaji ya madini ya chuma na nusu ya mahitaji yake ya protini kwa siku. Pia, mtoto atajipatia madini ya potasiamu, shaba na vitamin A, B na C.**

**Swali: Watu wengi wanapendelea kachumbari kama sehemu ya mlo. Je, iko salama?**

**Jibu:** Usalama wa kachumbari unategemea inavyotayarishwa. Ili iwe safi, ni muhimu kuiosha kwa maji safi. Mboga zinazotayarishwa kwa ajili ya kachumbari na zinachovywa kwenye maji moto kuua vijidudu. Baada ya hapo,zikatwe na kuchanganywa tayari kwa kuliwa.

**Swali: Kwa nini muhimu kufunika mboga za majani wakati wa kupika?**

**Jibu:** Ni muhimu, kwani inazuia upotevu wa vitamini zilizoko kwenye mboga. Mboga za majani zina virutubishi vingi, ikijumuisha vitamini mbalimbali.

Kwa kuwa vitamini huyeyuka kwenye maji, inaweza kupotea kwa njia ya mvuke kama hazikufunikwa.

**Swali: Je, mtu anajiepushaje na uzito mkubwa kupita kiasi?**

**Jibu:** Ziko njia za kujiepusha na uzito mkubwa kupita kiasi nazo, kama: Kupunguza ulaji vyakula vyenye mafuta mengi; kula vyakula vilivyopikwa kwa mvuke, kuchemshwa au kuokwa, badala ya vinavyokaangwa kwa mafuta; kupunguza vinywaji vilivyoongezwa sukari nyingi; ulaji matunda na mboga; na kufanya mazoezi ya kila mara, kulingana na afya yako.

**Swali: Watu wengi wanatumia soya kama kinywaji na katika utayarishaji wa baadhi ya vyakula. Je, ina faida gani mwilini?**

**Jibu:** Soya ni chanzo kizuri cha protini mwilini. Pili, maziwa ya soya yanakaribiana sana na ya wanyama tunayotumia. Hivyo, soya ni chakula chenye faida kubwa hasa kwa watu wasio na uwezo wa kupata vyakula vyenye asili ya wanyama.

**Swali: Je, matumizi ya ndimu na limau husababisha upungufu wa damu?**

**Jibu:** Matumizi ya ndimu na limau hayasababishi upungufu wa damu mwilini. Kinyume chake, ndimu na limau ni matunda yenye vitamin C yanayosaidia ufyonzwaji madini ya chuma yanayopatikana kwenye vyakula.

Madini ya chuma ni muhimu kutengenezea chembe nyekundu za damu. Kwa hiyo, ndimu na limau zinasaidia kuongeza na si kupunguza damu mwilini.

Ifahamike, ndimu na limau zinasaidia kuongeza hamu ya kula, hasa kwa mtu anayepata kichefuchefu na kutapika.

**Swali: Je, mmea wa mlonge una manufaa kilishe?**

**Jibu:** Mlonge ni mti unaokuwa haraka. Mmea huu huota vizuri katika maeneo ya joto, pia unastahimili ukame. Kila sehemu ya mmea huo, una thamani kama chakula.

Mbegu zake huliwa kama karanga huko (Bara) Asia na mafuta yatokanayo na mbegu, hutumika kupika na kutengeneza sabuni. Mizizi yake inaliwa kama ming'oko inayoliwa Mtwara.

Kabla mbegu hazijakomaa, ganda lake inaliwa kama maharage machanga na maua, inaweza kuliwa au kutumiwa kutengeneza chai. Majani ya mlonge, yanaliwa kama mboga, kwenye saladi, kitoweo, achari au kiungo kwenye chakula.

Mlonge kwa ujumla, una umuhimu kilishe kwa jamii. Mfano,mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja hadi mitatu akitumia gramu 100 za majani yalipikwa, atajipatia mahitaji yake yote ya madini ya chokaa.

Asilimia 75 ya mahitaji ya madini ya chuma na nusu ya mahitaji yake ya protini kwa siku. Pia, mtoto atajipatia madini ya potasiamu, shaba na vitamin A, B na C.

Mjamzito na mama anayenyonyesha, wanajipatia theluthi moja au zaidi kwa mahitaji yake ya madini chokaa, chuma, protini, shaba na salfa anayohitaji kwa siku.

Ni muhimu kuendelea kuzingatia ulaji vyakula mchanganyiko, ili kupata virutubishi muhimu vinavyohitajika mwilini, kwani hakuna chakula pekee kinachotosheleza mahitaji yote.

**Swali: Ni wakati gani mzuri kunywa maji; kabla, baada au wakati wa kula chakula?**

**Jibu:** Hakuna muda maalumu. Hata hivyo, inashauriwa kunywa maji baada ya mlo au kati ya mlo





Mlo unaojumuisha nyama ya kuku na limao, ambazo zimo katika kundi la nyama nyeupe.



Mtu akipata mlo.



Mtindi, moja ya lishe bora inayomfaa sana mwenye VVU na Ukimwi.



Kitunguu swaumu.

na mlo. Kunywa maji kabla ya mlo, kuwaweza kumnyima mtu nafasi ya kula chakula cha kutosha, ili kukidhi mahitaji ya virutubishi vyake.

**Swali: Je, wenye Ukimwi wanashauriwa kunywa maji?**

**Jibu:** Watu wanaoishi na VVU na wenye Ukimwi wanashauriwa kunywa maji kwa wingi, angalau lita moja na nusu kwa siku, kusaidia uyeyushwaji chakula na usafirishaji virutubishi mwilini.

Pia, maji yanasaidia kuondoa uchafu na kemikali zisizotakiwa mwilini. Vinywaji vingine vinavyochangia kuongeza maji mwilini ni juisi ya matunda, madafu, maziwa na supu.

**Swali: Wenye Ukimwi na virusi vyake, wanashauriwa au kuruhusiwa kunywa pombe?**

**Jibu:** Watu wanaoishi na VVU au wenye Ukimwi na wenye magonjwa mengine, hawashauriwi kunywa pombe, kwani inamfanya kukosa hamu ya kula.

Vilevile pombe, huingilia mchakato wa metaboliki mwilini. Unywaji pombe ulifanya ini kuharibika, hivyo kushindwa kufanya kazi yake ya kuondoa sumu mwilini.

Pombe inaingilia mfumo wa fahamu, hivyo kunapunguza uwezo kufikiri na maamuzi sahihi, kama vile ngono salama.

**Swali: Kuna tofauti gani, kati ya nyama nyekundu na nyeupe?**

> **Tofauti iliyopo kati ya nyama nyekundu na nyeupe inaonekana zaidi katika umeng'enywaji tumboni. Nyama, nyeupe inameng'enywa kirahisi, ikilinganishwa na nyekundu.**

**Jibu:** Nyama nyekundu ni za ng'ombe, mbuzi, kondoo na wanyama wengine wakubwa, tofauti na kuku, samaki na jamii yote ya ndege huwa na nyama nyeupe.

Tofauti iliyopo kati ya nyama nyekundu na nyeupe inaonekana zaidi katika umeng'enywaji tumboni. Nyama, nyeupe inameng'enywa kirahisi, ikilinganishwa na nyekundu.

Watu wenye Ukimwi wana matatizo ya uyeyushwaji na ufyonzwaji chakula mwilini. Iwapo watatumia nyama nyekundu, watapaswa kuiboresha, ili iweze kumeng'enywa kwa ufasaha.

Njia zinazoshauriwa kuifanya nyama nyekundu imeng'enywe kirahisi ni: Kutafuna kwa muda mrefu au kutumia nyama iliyosagwa; kuipika nyama kwa kutumia viungo vinavyosaidia kuilainisha, kama vile papai, limau, vitunguu saumu, na tangawizi au kula nyama na papai.

**Swali: Kuna chakula kinachopaswa kuliwa na wanaotumia dawa kupunguza makali ya Ukimwi?**

**Jibu:** Hakuna chakula maalumu kinachopaswa kuliwa na watu wanaotumia dawa za kupunguza makali ya Ukimwi. Hata hivyo, chakula ni muhimu, kwani husaidia dawa kufanya kazi kwa ufanisi.

Hata hivyo, kuna baadhi ya vyakula vinaingiliana na matumizi ya dawa mwilini. Hivyo, ni muhimu kuzingatia ushauri wa mtaalamu wa afya kuhusu matumizi ya dawa na chakula.

**Swali: Mtu anayeishi na virusi vya Ukimwi, anaweza kutumia mlo wenye pilipili?**

**Jibu:** Anaweza kutumia, ingawa yashauriwa itumike kwa kiasi kidogo. Iwapo ana vidonda mdomoni au kooni au ikiwa anaharisha, hashauriwi kutumia pilipili kabisa, inazidisha maumivu ya vidonda.

Pia, pilipili kutokana na mwasho wake, husababisha usumbufu tumboni, hivyo kuzidisha hali ya kuharisha.

**Swali: Ni kweli kwamba, mwenye Ukimwi haruhusiwi kutumia sukari?**

**Jibu:** Sukari ni chanzo kimojawapo cha nishati kinachoupatia mwili nguvu na joto. Kila mtu anashauriwa kutumia kiasi kidogo cha sukari.

Hata hivyo, wanaoishi na virusi vya Ukimwi na wenye Ukimwi, wanapokuwa na fangasi kinywani au kooni, wanashauriwa kupunguza matumizi ya sukari. Hii ni kwa sababu sukari huchochea kukua fangasi, hivyo kuongeza tatizo.

**Swali: Kuna madhara yoyote yanayompata mtu anayeishi na virusi vya Ukimwi, anapokuwa na uzito mkubwa kupita kiasi?**

**Jibu:** Wenye uzito mkubwa kupita kiasi, wana hatari zaidi ya kupata matatizo ya moyo na shinikizo la damu. Pia, uzito mkubwa ni kati ya sababu zinazochangia mtu kupata ugonjwa wa kisukari.

Anayeishi na VVU au Ukimwi, anashauriwa awe na uzito wa wastani. Ufafanuzi wa uzito wa kadiri waweza kutolewa na wataalamu wa afya au lishe.

**Swali: Kuna ulazima kwa anayeishi na VVU, kutumia virutubishi vya nyongeza?**

**Jibu:** Anayeishi na VVU au mwenye Ukimwi, halazimiki kutumia virutubishi vya nyongeza. Jambo la msingi ni kula chakula cha kutosha na mchanganyiko wa makundi yote ya vyakula.

Ulaji chakula cha kutosha na mchanganyiko, unaupatia mwili virutubishi vinavyohitajikai. Endapo mtu anataka kutumia virutubishi vya nyongeza, ni muhimu kupata ushauri wa mtaalamu wa afya kwanza.

**Swali: Watu wanaoishi na VVU wanashauriwa kutumia maziwa ya mtindi. Je, una faida gani kwao?**

**Jibu:** Mtindi humeng'enywa kwa urahisi zaidi mwilini ikilinganishwa na maziwa mabichi (fresh). Pia mtindi husaidia umeng'enywaji na ufyonzwaji wa virutubishi vinavyopatikana kwenye vyakula vingine.

Watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi hupata matatizo ya umeng'enywaji na ufyonzwaji wa virutubishi mwilini, hivyo mtindi huwa na faida kwao.

**Swali: Je, kitunguu swaumu kina faida gani kwa mgonjwa wa Ukimwi?**

**Jibu:** Mara nyingi wenye Ukimwi, wanasumbuliwa na maambukizi mbalimbali. Kitunguu swaumu kina uwezo wa kuua bakteria, virusi na fangasi hususan tumboni, katika mapafu na ukeni.Kinasaidia kutibu utando kinywani, maambukizi katika koo, malengelenge ya ngozi na kuharisha. Pia, inasaidia umeng'enyaji chakula tumboni.

**Swali: Ni ni nini umuhimu wa asali kwa wenye Ukimwi?**

**Jibu:** Asali ina nishati kwa wingi. Pia ina virutubishi vingine kama utomwili (protini), vitamin na madini. Asali imeonesha kufanya kazi kama kiua vijasumu (antibiotic).

Hivyo huweza kutumika kutibu kikohozi, fangasi kinywani na vidonda ambapo ni pamoja na vidonda vya mdomoni na kooni. Hata hivyo, yashauriwa kusukutua kinywa kila mara, baada ya kula asali, ili kuondoa mabaki ya sukari yanayoweza kuleta madhara.

**Swali: Kuna watu wanaosaga mboga mbichi za majani, kupata juisi. Je, kuna madhara yanayoweza kumpata anayeishi na VVU kwa kutumia juisi hiyo?**

**Jibu:** Kutumia juisi itokanayo na mboga mbichi, kunaweza kuwa na athari, pale usafi wa mboga na maji yanayotumika. Ili juisi iwe salama, ni muhimu kuosha mboga kwa maji safi na kisha kuchovya kwenye maji ya moto, kuua vijidudu kabla ya kuzisaga..

***Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa simu: (+255) 0784 334 096 au barua pepe: marobarnabas@yahoo.com***

AFYA

# Wanaume 43, 000 kufanyiwa tohara mkoani Shinyanga



Muelimishaji kuhusu tohara mkoa wa Shinyanga, Nchama Samson, akiwa kazini.

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

KUFANYIKA tohara kwa wanaume, ni moja ya njia za kinga kuzuia maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU), ikionyesha mafanikio kwa asilimia 60.

Wadau wa afya kwa kushirikiana na serikali, wamekuwa wakiendesha kampeni hiyo ya tohara kwa wanaume katika mikoa mbalimbali nchini, ikiwamo Shinyanga, lengo ni kupunguza kasi ya maambukizi ya virusi hivyo vya Ukimwi.

Wataalamu wa afya wanasema kwamba, mwanamume aliyefanyiwa tohara anakuwa katika ngazi ya kinga kwa asilimia 60 kutopata maambukizi ya virusi hivyo, wakati wa kufanya tendo la ndoa, kuliko yule ambaye hajatahiriwa anayekuwa na asilimia 100 ya maambukizi.

Shirika la Itrahealth liko katika kampeni ya kuhamasisha wanaume kujitokeza kufanyiwa tohara bure, ili kuweza kukijinga kupatwa na maambukizi ya virusi hivyo vya ukimwi.

Miongoni mwa mikoa ambayo shirika hilo linaendesha kampeni zake ni Shinyanga, ambako lilianza kazi hiyo mwaka 2011 na kufanikisha kutahiri wanaume 64,000.

Mwaka huu, shirika hilo limeanza tena kampeni ya kuhamasisha wanaume kujitokeza kufanyiwa Tohara katika halmashauri tano za mkoa wa Shinyanga, ambazo ni: Kahama Mji, Ushetu, Msalala, Shinyanga Vijijini na Manispaa ya Shinyanga.

Msafiri Swai, ni mratibu wa shughuli za kuhamasisha kampeni za tohara kwa wanaume Shinyanga kutoka Itrahealth, anayesema malengo tarajiwa katika halmashauri hizo tano za mkoa wa Shinyanga hadi kufikia Oktoba mwaka huu ni kutahiri wanaume 42,894.



Shughuli za tohara zikiendelea. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> Tunaomba pia hili liwe linafanywa kwa usiri na siyo watu wazima kuchanganywa na watoto. Tutengewe vyumba vyetu, pamoja na kupewa madaktari wa kiume.

Anasema kazi ya kutahiri wanaume, lilianza Oktoba 2018 na linatarajiwa kuhitimishwa Oktoba. Kwa sasa wanaendelea na kampeni hiyo ya kuhamasisha tohara kwa wanaume, wakishirikiana na viongozi wa serikali, wakiwamo watendaji vijiji, kata na Sungusungu.

Anabainisha kuwa katika Halmashauri ya Kahama Mji, lengo ni kutahiri wanaume 10,646, lakini mpaka sasa wameshatahiri 1,365.

Msalala, lengo ni kuwafikia wanaume 17,805 na waliotahiriwa hadi sasa ni 2,120; Ushetu inalenga 10,642 na waliofanyiwa Tohara ni 2,617. Katika Halmashari ya Shinyanga Vijijini wanalengwa 3,219 na waliotahiriwa ni 418, huku katika Manispaa ya Shinyanga, wanalengwa 582 na waliotahiriwa 90.

"Kwa takwimu hizi kasi yake ni ndogo ya kufanikisha kufikia malengo ambayo tumeweka ya kutahiri wanaume 42,894 kwa mwaka. Mpaka sasa tumeshatahiri wanaume 6,610 na juhudi bado zinahitajika zaidi, kuhamasisha wanaume kujitokeza kwa wingi kufanyiwa Tohara," anasema Swai.

"Unapotahiri wanaume wengi kwa muda mfupi, ndipo unapofanikiwa kupunguza kasi ya maambukizi haya ya virusi vya Ukimwi, kuliko kwenda kwa kasi ndogo, tutakuwa hakuna tunachokifanya na maambukizi yataendelea kushika kasi," anaongeza.

### MWENYEKITI USHETU

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ushetu, Juma Kimisha, anasema sehemu ambayo kwa sasa kampeni ya tohara ndipo inafanyika, anasema kazi hiyo imekuwa ikisuasua kwa sababu ya kuwapo imani potofu, kwamba mwanamume ambaye umri umekuwa mkubwa, akifanyiwa tohara anapungukiwa na nguvu za kiume.

Anasema jamii ya wakazi wa mahali hapo, hawapendi kufanyiwa tohara kutokana na utamaduni walioukuta kutoka kwa wazazi wao, hali ambayo imekuwa ikisababisha kusuasua na kuanza kupandikizwa maneno ya imani potofu.

"Tatizo kubwa ambalo limekuwa likikwamisha tohara kutofanikiwa kwa asilimia 100, ni kuwapo maneno ya imani potofu ambayo yanasambazwa kwa wanaume huko vijijini, kuwa mwanaume akifanyiwa tohara ukubwani utapungukiwa na nguvu za kiume.

"Kazi ambayo sisi kama wanasiasa, viongozi wa serikali mkiwamo watendaji wa kata, vijiji na wataalamu wa afya, ni kwenda kutoa elimu ipasavyo kwa wanaume juu ya umuhimu wa tohara kwao, ili kutokomeza imani hiyo potofu, ndipo tutafanikiwa kufikia malengo ya kutahiri wanaume wengi," anaongeza.

### MTENDAJI KATA

Mathew Francis, ni Mtendaji Kata wa Idahina wa Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama, anasema tatizo hilo la imani potofu limekuwa moja ya chanzo cha kukwamisha tohara, kwa kuwa na mikusanyiko ya wanaume wanaopeana maneno ya uongo kuhusu tohara, kwamba ni tatizo kwa watu wazima.

"Mimi nimekuwa nikishuhudia mikusanyiko ya wanaume kwenye 'masenta' wakiambiana maneno ya uongo, kuwa mwanaume ambaye umri umekwenda akifanyiwa tohara lazima nguvu za kiume zipungue, maumbile kuwa madogo pamoja na performance kushuka,"anasema Francis.

### ASIYEFANYIWA TOHARA

Hamisi Mayombo, ni mkazi wa Ushetu ambaye hajafanyiwa tohara, anayesema kuwa yeye baada ya kusikia madai hayo potofu kuhusu tohara aliogopa, lakini elimu aliyepatiwa kuhusu faida za tohara kuhusiana na Ukimwi, ameahidi kwenda kufanyiwa.

"Tunaomba pia hili liwe linafanywa kwa usiri na siyo watu wazima kuchanganywa na watoto. Tutengewe vyumba vyetu, pamoja na kupewa madaktari wa kiume. Tumekuwa tukiogopa kwenda kutahiriwa kwa sababu ya kuogopa fedheha kutoka kwa wanawake, endapo nikigundulika nimekwenda kutahiriwa," anasema Mayombo.

### MRATIBU MRADI

Mratibu wa Kudhibiti Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi, katika Halmashauri ya Ushetu, Mogani Mwita, anataja takwimu za maambukizi ya ugonjwa huo ni asilimia 2.4, hali ambayo siyo ya kuridhisha na kuifanya kuhitajike juhudi za wanaume kupewa elimu ya tohara pamoja na kuacha ngono zembe.

Anasema, tatizo ambalo limekuwa likichochea kasi hiyo ya maambukizi hayo ya VVU, ni kuwapo mikusanyiko mikubwa ya kwenye baadhi ya maeneo kama magulio hadi usiku, kwenye ngoma za asili kipindi cha mavuno ya mazao na mwingiliano wa watu kwenye mashamba ya tumbaku.





# Watoto wanaoishi mazingira magumu pasua kichwa

**Na Mwanbdishi Wetu,** MBEYA

MKOA wa Mbeya bado unaendelea kukabiliwa na ongezeko la watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi, huku migogoro ndani ya ndoa imetajwa chanzo cha ongezeko hilo.

Hayo yalisemwa jana na Mrakibu wa Jeshi la Polisi ambaye pia ni Mratibu wa Dawati la Jinsia na Watoto mkoani Mbeya, Janeth Masagano, alipokuwa akizungumza na Nipashe ofisini kwake, alisema wimbi la watoto wa mitaani linaendelea kuongezeka mkoani Mbeya kutokana na migogoro iliyopo kwenye familia baina ya baba na mama.

Alisema migogoro ya wazazi kugombana au kuachana imesababisha watoto kuzikimbia familia zao na kwenda kutafuta amani na upendo, matokeo yake hulazimika kuishi kwenye maeneo hatarishi.

"Migogoro ndani ya familia ni chanzo cha matatizo ambayo yamechangia wimbi la watoto wa mitaani, watoto hulazimika kukimbia ili kutafuta amani sehemu nyingine na huko wanakokimbilia hukutana na watoto wengine, matokeo yake hufundishana vitendo viovu," alisema Janeth.

Alisema mara kadhaa ameshuhudia wimbi kubwa la watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi kwenye maeneo mbalimbali ya maficho, alisema baadhi ya watoto waliohojiana nao walisema wamezikimba familia zao kwa sababu ya migogoro na vipigo wengine wakisema hawako tayari kurejea makwao.

Aliongeza kuwa katika kuadhimisha kilele cha Siku ya Wanawake Duniani, Janeth alidai vitendo vya ukatili wa kijinsia kama ubakaji na ulawiti vinaendelea kuripotiwa kwa maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya.

Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Februari, mwaka huu, jumla ya kesi 20 ya vitendo vya ubakaji na ulawiti viliripotiwa.

Alisema katika ripoti hiyo idadi ya watoto kufanyiwa vitendo hivyo ni kubwa ukilinganisha na watu wazima, huku akitaja sababu kuwa ni kinamama kujikita kwenye shughuli za uzalishaji kuliko kutoa malezi kwa watoto wao.

Baadhi ya wazazi wamekuwa sio wasimamizi wazuri wa watoto wao badala yake wanajikita zaidi kwenye shughuli za kiuchumi na kuwaachia wafanyakazi wa ndani kutimiza jukumu hilo.

"Tunapoadhimisha siku hii ikiwa na kauli mbiu ya 'Badili fikra kufikia maendeleo endelevu,' tuhakikishe kila mzazi anawajibika lazima awe mlinzi na mlezi bora wa familia, kwanza itasaidia kutengeneza kizazi chenye maadili na wazalendo hapo baadaye," alisema Janeth.

Baadhi ya kinamama mkoani Mbeya walisema kuwa bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika kutafuta fursa za kujiongezea kipato.

Mmoja wa wanawake hao, Beatrice Mwakipesile ambaye ni mkazi wa mtaa wa Mama John, alisema miongoni mwa changamoto hizo ni rushwa ya ngono wanapohitaji nafasi za kazi au uongozi.

# Naibu Waziri aipa kibarua kigumu hospitali ya rufani Mbeya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mussa Sima, ameagiza kujengwa mtambo maalum wa kisasa kwa ajili ya kuchomea taka hatarishi katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya ili kukabiliana na athari za kimazingira na kulinda afya za wananchi. Alitoa agizo hilo hivi karibuni alipotembelea eneo la kuchomea taka hatarishi katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya, ambapo alionyesha kutoridhishwa na hospitali hiyo kukosa mtambo maalumu wa kuchomea taka hatarishi.

Alisema hospitali hiyo haina mtambo maalum wa kuchomea taka hatarishi na badala yake taka hatarishi huchomwa kwenye shimo ambalo halijawekewa miundombinu rafiki ya kukabiliana na moshi.

Aliongeza kuwa eneo la kuchomea taka hizo lipo karibu na Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Loleza na kwamba wako hatarini kukumbwa na magonjwa kama vile saratani kutokana na moshi.

Alisema kwa hadhi ya hospitali hiyo taka hatarishi zisingechomwa kwenye shimo kama inavyofanywa kwenye zahanati na vituo vya afya, badala yake watengeneze mtambo maalum ambao utachoma taka hizo. "Hospitali inatumia shimo kuchoma taka, mbaya zaidi sehemu yenyewe haijafunikwa kwa hiyo moshi unaotoka hapo unasambaa kwenye makazi ya watu ikiwamo Shule ya Wasichana ya Loleza, nimetoa maelekezo kuwa waweke mkakati madhubuti na haraka watengeneze chemba za kuingiza na kuchomea taka wakati wakijiandaa na mkakati wa kutengeneza mtambo maalum," alisema Naibu Waziri Musa.

Akizungumzia maagizo hayo, Kaimu Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. Paul Lawala, alisema kuwa tayari maagizo yametekelezwa ambapo wameweza kutenga chemba na kuboresha miundombinu ya kuchomea taka hizo. Alisema tayari wanaendelea kuboresha miundombinu ya kuchomea taka hatarishi lakini pia wanafanya jitahada za kutafuta fedha ili kutengeneza mtambo maalum na wa kisasa wa kuchoma taka hizo. "Tulibaini baadhi ya changamoto katika eneo hili la kuchomea taka na tulianza mchakato wa kutafuta fedha, ambapo gharama yake ni kubwa kwa sababu katika mtambo huo lakini tutafute gesi au nishati ya umeme ambayo itakuwa inachoma taka hizo alisema Dk. Lawala.



Mkuu wa Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Sarah Chiwamba (kulia), akipeana mkono na Meneja wa Kitengo cha Biashara za Serikali wa NMB Kanda ya Kusini, Haji Msigwa (wa pili kushoto), ikiwa ni ishara ya kukabidhiwa mabati 167 yenye thamani ya shilingi milioni 5 kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Sekondari Nangano, katika hafla iliyofanyika wilayani humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Hasunga atangaza neema kwa wakulima

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

SERIKALI ipo kwenye mchakato wa kuanzisha bima ya mazao kwa wakulima ambayo itamsaidia kupata fidia pindi atakapopata majanga ikiwa mazao yake yataharibika kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Kauli hiyo ilitolewa juzi jijini Mbeya na Waziri wa Kilimo na Ushirika, Japhet Hasunga, wakati wa uzinduzi wa ushirikiano kati ya Mradi wa USAID -NAFAKA, na kampuni ya kimataifa ya Marekani ya uzalishaji na usambazaji mbegu na viuatilifu (Corteva).

Waziri Hasunga alisema wakulima wamekuwa wakipata hasara baada ya mazao yao kuharibiwa na mafuriko, ukame pamoja na viwavijeshi licha ya kutumia gharama kubwa ya uzalishaji.

Alisema serikali imeona changamoto hiyo na kwamba iko kwenye mkakati wa kuanzisha bima ya mazao kwa wakulima ambayo itakuwa mkombozi wakati wa majanga hayo.

"Bima ya mazao itakuwa kifuta jasho kwa wakulima nchini badala ya kulia watakapopata majanga ya kuharibikiwa na mazao yao, wao watacheka kwa sababu watalipwa fidia," alisema Waziri Hasunga.

Alisisitiza wakulima kujisajili kwa wingi bima hiyo itakapoanzishwa kwa madai kuwa itasaidia kuendeleza shughuli za uzalishaji pamoja na kuanzisha kazi nyingine za kujiingizia kipato.

Aidha, Waziri Hasunga alisema serikali iko kwenye maandalizi ya mwisho ya kujenga kiwanda kikubwa za viuatilifu mkoani Mbeya ambacho kitahudumia wakulima wote wa Nyanda za Juu Kusini.

Alisema sababu ya kujenga kiwanda hicho mkoani Mbeya ni kutokana na uhitaji mkubwa wa matumizi ya viuatilifu hivyo ukilinganisha na maeneo mengine.


"Tanzania tunazalisha pembejeo kwa asilimia 10 tu na asilimia nyingine 60 tunategemea kutoka nje ya nchi, tunatumia gharama kubwa kuagiza pembejeo ndio maana tunaendelea kujenga na kuanzisha viwanda mbalimbali vya kuzalisha mbegu na viuatilifu ili wakulima wetu wazipate kwa wakati na gharama nafuu," alisema Hasunga.

Mkurugenzi wa Ukuaji wa Uchumi kutoka Shirika la USAID - NAFAKA, Terhi Majanen, alisema wataendelea kushirikiana na serikali katika kutoa elimu ya kilimo bora pamoja na kuwaunganisha na taasisi za kifedha ili waendelee kunufaika na kilimo.

Pia alieleza kuwa lengo la mradi huo ni kuwasaidia wakulima kupata mbegu na pembejeo sahihi ili waweze kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao.

Mmoja wa wakulima hao kutoka Kijiji cha Ivwanga wilayani Mbozi, mkoani Songwe, Joseph Mwampashi, alisema kuwa serikali na wadau wengine bado haijafanikiwa kukabiliana na wimbi la uzalishaji wa mbegu feki.

Alisema changamoto hiyo imewasababishia hasara wakulima wengi kwa sababu ya kutokuwa na elimu ya kutambua mbegu feki, aliiomba serikali na wadau kudhibiti mianya ya uzalishaji na uingizwaji wa mbegu hizo nchini.





# Mavunde ataka iwekwe mikakati kuimarisha ulinzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, amesema kutokana na Jiji la Dodoma kukua kwa kasi, inahitajika kuongeza matumizi ya teknolojia hasa kwenye maeneo ya ulinzi na usalama.

Mavunde aliyasema hayo jana alipokuwa akizindua ofisi ya kampuni ya G-Tech inayojishughulisha na masuala ya teknolojia ya habari na mawasiliano, jijini hapa.

Alisema baada ya maamuzi ya Rais John Magufuli ya kuifanya Dodoma kuwa makao makuu ya nchi na kupata hadhi ya jiji hivi sasa inakua kwa kasi.

"Hivi kutokana na kukua kwa kasi inatakiwa maendeleo yake yaendane na ukuaji wa teknolojia, hasa kwenye maeneo ya ulinzi na usalama, hivyo tunaimani uwepo wenu mtasaidia kutoa huduma hii," alisema.

Alisema uwekezaji huo umekuja wakati mwafaka na serikali inaunga mkono jitihada zinazofanywa na vijana.

Aidhaalisema kwa sasa serikali inaangalia kupitia mfuko wa maendeleo ya vijana kusaidia kijana mmoja mmoja badala ya vikundi.

"Mfuko huu awali ulikuwa unalenga vikundi na Saccos sasa tunaangalia utaratibu wa mtu mmoja mmoja ambaye akipata msaada atasaidia na vijana wenzake kuliko utaratibu wa hivi sasa kuhangaika na kikundi cha watu wengi na kushindwa kufikia matarajio," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Salim Mussa Omary, alisema kamera husaidia kuimarisha ulinzi na usalama majumbani na maofisini.

Alifafanua kuwa kampuni hiyo imejikita kutoa huduma za habari na mawasiliano na pia ilishiriki katika uwekaji wa kamera za CCTV barabara za Zanzibar. Alisema asilimia 80 hadi 90 ya wateja waliopo Zanzibar ni serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

"Kwa hali hii inaonyesha vijana wa ndani wazalendo tunaweza, leo tupo Dodoma kampuni hii imekuja ili kuhakikisha kunakuwa na usalama," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema matumizi ya kamera yanasaidia kwenye masuala ya uchunguzi.



Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Fortunatus Muslim, (katikati), akiongoza askari wa kikosi hicho kufanya ukaguzi wa moja ya lori linalofanya safari zake nje ya nchi katika mizani ya Mikumi iliyopo wilayani Kilosa jana. Kulia ni Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Morogoro, Michael Deleli. **PICHA: ASHTON BALAIGWA,**

# Katambi aagiza wasakwe waliowapachika mimba wanafunzi 40

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, amemwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD), kuhakikisha wanawakamata wahusika wote waliowapa ujauzito wanafunzi zaidi ya 40 kutoka shule za sekondari 10 zilizopo jijini hapa.

Katambi alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akitoa taarifa ya wilaya katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma. Alisema wanafunzi hao walipata ujauzito katika kipindi cha mwaka huu wa masomo na hivyo kulazimika kukatisha masomo yao.

Aliongeza tatizo hilo limekuwa ni kikwazo cha kufikia lengo la serikali la kutoa elimu bure kwa watoto, lakini pia linamnyima fursa mtoto ya kupata haki ya msingi ya kupata elimu. "Kwa tatizo hili hata malengo yetu ya kiafya hatuwezi kuyafikia katika kuhakikisha kunakuwa na ustawi kwa watoto wadogo wanaozaliwa kwa sababu mama ni mtoto anazaa tena mtoto mwingine, huu unakuwa mzigo juu ya mzigo, natoa agizo kwa OCD awasake na kuwakamata wahusika wote waliofanya kitendo hiki," alisema Katambi.

Alisema wanafunzi hao waliopata ujauzito wengi ni wa kidato cha pili, tatu na kidogo kidato cha nne.

Alitaja kuwa wanafunzi hao wanatoka katika Shule ya Sekondari Mtumba, Chikole, Makutupora, Chigongwe, Mpunguzi, Ihumwa, Hazina na Chinangali.

"Na kwa bahati mbaya kati ya wanafunzi hao, mmoja amepimwa amekutwa ameshaambukizwa virusi vya Ukimwi, hili haliwezekani lazima tuwasake wahusika," alisisitiza Katambi.

Katambi alisema pamoja na halmashauri kuweka mipango yake mizuri, changamoto itakuwapo katika utekelezaji endapo wataruhusu hali hiyo iendelee kutokea.

# Vitambulisho 11,000 vya wajasiriamali kutolewa Ikungi

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

WILAYA ya Ikungi mkoani Singida imeweka mpango mkakati wa kuhakikisha ifikapo Machi 28, mwaka huu iwe imekamilisha ugawaji wa vitambulisho 11,000 kwa wafanyabiashara wadogo vilivyotolewa na Rais John Magufuli hivi karibuni.

Akizungumza na Nipashe jijini hapo, Mkuu wa Wilaya, Miraji Mtaturu, alisema mkakati huo utafanikiwa baada ya kushusha ugawaji wa vitambulisho hivyo kwa watendaji wa kata ambao wao ni rahisi kuwafikia na kuwatambua wafanyabiashara hao.

Alibainisha kuwa awamu ya kwanza walikabidhiwa vitambulisho 3,000 na awamu ya pili walipewa vitambulisho 8,000.

"Tulichofanya tumeshusha vitambulisho kwa watendaji wa kata ili kurahisisha zoezi hilo na kuwatambua kwa haraka, hapa Ikungi tuna kata 28, kila mtendaji tumempa vitambulisho mia moja ingawa wengine tumewapa mia mbili kulingana na eneo lake," alisema Mtaturu.

Alisema mpaka sasa wameshagawa vitambulisho 1,071 na wanaendelea ili kufikia lengo lililopo.

Mkuu huyo alisema kwa mujibu wa maelekezo waliyopewa na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, wanatakiwa kukamilisha ifikapo Machi 28, mwaka huu.

Hata hivyo, alisema changamoto waliyokumbana nayo mpaka sasa ni maelekezo waliyoyapata awali ya kutoa vitambulisho kwa wafanyabiashara hao wasio na namba ya mlipa kodi(TIN), ilhali wengine walikuwa nazo kwa ajili ya kupata mikopo au kumiliki bodaboda na sio kulipa kodi.

Kutokana na hilo, Mtaturu alisema kama wilaya wanaendelea kutoa elimu juu ya hilo ili kutokwamisha zoezi hilo.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara hao kujitokeza kujiandikisha ili wapate vitambulisho hivyo ambavyo havina urasimu kwa gharama ya Sh. 20,000.

## HABARI ZANZIBAR



# Teknolojia ya mawasiliano ya simu yaokoa familia za wavuvi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KUIMARIKA kwa huduma ya mawasiliano ya simu kumesaidia kupunguza tatizo la utelekezwaji wa wanawake na watoto katika kisiwa cha Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Akizungumza na waandishi wa habari msimamizi wa kamati ya malezi mbadala Shehia ya Tumbatu Jongowe, Juma Sharif Hassan, alisema hivi sasa wavuvi wa kisiwa hicho wanapoenda kuvua nje ya kisiwa hicho wamekuwa wakituma pesa kupitia mitandao ya simu za mkononi kwa ajili ya mahitaji mbalimbali kwa familia zao.

Alieleza kuwa miaka ya nyuma wavuvi wa kisiwa hicho wanapoenda katika shughuli zao za uvuvi walikuwa wakizitelekeza familia zao zaidi ya miezi mitatu bila ya huduma yoyote.

Alisema kutokana na elimu inayotolewa ya masuala ya udhalilishaji na malezi mbadala hivi sasa wavuvi hao wamekuwa wakituma pesa za matumizi kwa familia zao kupitia mitandao ya simu za mkononi.

"Watoto wa kisiwa hiki walikuwa wakikabiliwa na tatizo kubwa la utapia mlo kwa sababu kinababa wanapoenda katika shughuli za uvuvi (dago) huzitelekeza familia zao na huwepo nje ya Zanzibar kama Tanga, Bagamoyo na maeneo mengine, huku watoto wakiwa hawana chakula," alisema Juma.

Aidha, alieleza kuwa bado wananchi wa kisiwa hicho wametawaliwa na mfumo dume kwa kuwa anapojitokeza mwanamke na kuripoti matukio ya udhalilishaji hutengwa na jamii.

Alieleza kuwa wapo baadhi ya wanawake hudhalilishwa kijinsia na waume zao, aidha, kupigwa au kutelekezwa lakini wanapojaribu kuripoti katika uongozi wa shehia hutengwa na jamii.

"Kwa kweli kuendelea kufumbia macho vitendo vya udhalilishaji tutachelewa kupata maendeleo kisiwani kwetu, hivyo niiombe jamii ya watu wa Tumbatu kuondokana na muhali na kutoficiana maovu," alisema.

Kwa upande wake, Sheha wa Shehia ya Tumbatu Jongowe, Miza Ali Sharif alieleza kuwa utekelezaji mkubwa uliopo hivi sasa kisiwani humo ni baada ya kuvunjika kwa ndoa ambapo kinababa huwatelekeza wanawake na watoto.

Alieleza kwamba licha ya wanawake kukabiliwa na hali hiyo ya udhalilishaji kwa kutelekezwa na watoto baada ya ndoa kuvunjika, lakini wamekuwa wagumu kuripoti matukio hayo.

"Hii jamii ya watu wa Tumbatu ni ya wenyewe kwa wenyewe hakuna mtu mgeni kutoka nje ya kisiwa hiki sasa wanaoneana muhali (aibu) kuripoti matukio ya udhalilishaji lakini udhalilishaji upo hasa kwa wanawake na watoto," alisema.

Alieleza kuwa kuhusu wanaume ambao wamo katika ndoa kutelekeza familia zao kutokana na shughuli za uvuvi hilo limepunguwa kutokana na kuimarika kwa huduma ya mawasiliano ya simu za mkononi na wanapokuwa mbali na familia zao hutuma pesa kupitia mitandao hiyo.

Aidha, alieleza kuwa udhalilishaji mwingine uliopo kisiwani hapo ni utumikishaji kwa watoto ambapo hujishughulisha na shughuli za uvuvi wakati wa muda wa kupata elimu shuleni.

Alisema jiografia ya kisiwa hicho kimezungukwa na bahari, hivyo watoto hutoroka shule na kufanya shughuli za kujipatia kipato ikiwamo kubeba mizigo baharini na kuvua.



Wachuuzi wakipaa samaki kabla ya kuwauzia wateja katika soko la kimataifa la Feri jijini Dar es Salaam. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Wanawake wanaofanya kazi nje wafanyiwa udhalilishaji

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

IMEELEZWA kuwa kundi kubwa la wanawake wanaosafirishwa kwenda kufanya kazi nje kutokea visiwa vya Zanzibar wanakabiliwa na manyanyaso na kudhalilishwa kingono.

Kauli hiyo ilitolewa jana visiwani hapa na ofisa kutoka Shirika la Kimataifa la Wahamaji, Lena Lutengano.

Aliyasema hayo wakati akizungumza katika kongamano kuhusu Siku ya

Wanawake Duniani lililofanyika katika viwanja vya Kariakoo Mjini

Unguja, ambapo wadau mbalimbali wa masuala ya kutetea haki za wanawake na watoto walikutana.

Alisema kuwa wanapoondoka Tanzania wakiwa na imani wanaenda kufanya kazi za halali kwa ajili ya kujipatia kipato, lakini baada ya kufikishwa huko hutumikishwa kwa kufanyishwa kazi ambazo ni kinyume na maadili.

Alieleza kuwa kuongezeka kwa biashara za usafirishaji haramu wa binadamu kunasababishwa na mambo mbalimbali ikiwamo ukosefu wa ajira na umaskini, hivyo vijana huishia kudanganywa kwenda kufanya kazi nje ya nchi na kupata manyanyaso.

"Vitendo vya ukatili vya jinsia vikipitiliza watu wanajikuta kuwa wahanga wa usafirishaji wa binadamu,"alisema.

Naye Waziri wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Shadya Mohmed, alisema kuimarisha ubunifu wa mikakati iliyobora zaidi itakayoongeza kiwango cha maendeleo ya sayansi na teknolojia duniani

na kutasaidia kuleta mabadiliko a maisha ya wanawake wa mjini na vijijini.

Alisema wanawake wanapaswa kujengewa uwezo wa elimu, taaluma, ujuzi na rasilimali zinazoendana na wakati ili kuepukana na vitendo vya udhalilishaji.

Aliongeza kuwa licha ya wanawake kukabiliwa na changamoto nyingi hususani katika masuala ya udhalilishaji wa kijinsia lakini pia endapo watapewa fursa za kimaendeleo watafikia malengo endelevu yaliyokusudiwa.

# Uhaba wa mafuta waibuka Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

TATIZO la upungufu wa mafuta ya petroli umeanza kujitokeza tena visiwani Zanzibar, ambapo baadhi ya vituo vya kuuzia bidhaa hiyo vimeonekana kufungwa.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

Zanzibar, Haji Kali Haji, amesema upungufu huo wa mafuta umesababishwa na kampuni ya United Petroleum kushindwa kuingiza mafuta kwa wakati waliopangiwa.

Akizungumza na waandishi wa habari, ofisini kwake Maisara Mjini Unguja, alisema kuwa hali hiyo imesababisha kupungua kwa mafuta ya petroli kwa baadhi ya vituo.

Alieleza kuwa kampuni ya Zanzibar Petroleum pamoja na kampuni ya Gapco ndio waliyoingiza mafuta na yameanza kusambazwa na kuuzwa katika vituo hivyo.

Mkurugenzi huyo alisema wameipiga faini kampuni hiyo ya mafuta Dola za Marekani 20,000 kutokana na kuchelewa kuingiza mafuta hayo na watatakiwa kulipa ndani ya wiki mbili.

Alisema kwa sasa kiwango cha mafuta kilichoko katika kampuni ya Gapco lita 942,317 za petroli, dizeli lita, 799,629 na mafuta ya taa lita 213,305.

Kwa upande wa kampuni ya Zanzibar Petrolium ina akiba ya lita 407, 415 za petroli, dizeli 904,688 na mafuta ya taa 215,912, ambapo kampuni ya United Petroleum ina lita 98,152 za petroli, dizeli 205,505 na mafuta ya taa lita 472,194.

Mkurugenzi huyo alisema Kampuni ya Zanzibar Petroleum inatarajia kuingiza mafuta kiasi cha lita 1,600,000 za petroli kwa kutumia meli ya East Wind I Machi, 10 mwaka huu.

HABARI KIMATAIFA

# Mgomo wavuruga safari za ndege Nairobi

**NAIROBI,** Kenya

SHUGHULI za usafiri wa ndege zimevurugika katika Uwanja wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta (JKIA) nchini Kenya, kufuatia mgomo wa wafanyakazi wanaopinga usimamizi wa uwanja huo kuongozwa na Shirika la Usafiri wa Ndege ya Kenya (KAA).

Wasafiri wengi katika uwanja wa JKIA ambao unaongoza kuwa na shughuli nyingi zaidi katika eneo la Afrika chini ya Jangwa la Sahara, walikumbana na zogo la mgomo wa wafanyakazi wa uwanja huo.

Mgomo huo ulioanza usiku wa manane wa kuamkia jana, umeathiri shughuli katika viwanja vya ndege vya miji ya Mombasa, Kisumu na Eldoret kutokana na ndege kushindwa kusafiri kwa wakati.

Sababu kubwa ya mgomo huo ni wafanyakazi kupinga usimamizi wa uwanja huo kutwaliwa na KAA, ambapo walisema hatua hiyo itasababisha wengi wao kukosa ajira.

Katibu Mkuu wa chama cha wafanyakazi wa mashirika ya usafiri wa angani nchini Kenya, Moses Ndiema, muda mfupi kabla ya kukamatwa na polisi alisema: "Wafanyakazi wa uwanja huu ndio wamefanya hali kuwa hivi ilivyo, sisi ni wengi na wasipotupatia tutajichukulia, tumeweka misururu ya mikutano tukiwaambia waje tuongee, na kama leo wanataka tuongee waje hapa."

**Wafanyakazi wa uwanja huu ndio wamefanya hali kuwa hivi ilivyo, sisi ni wengi na wasipotupatia tutajichukulia, tumeweka misururu ya mikutano tukiwaambia waje tuongee, na kama leo wanataka tuongee waje hapa.**

Shirika la Ndege nchini Kenya, lina mipango ya kuingia ubia na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ili kuvisimamia viwanja vyote vya ndege nchini Kenya.

Juzi, Waziri wa Uchukuzi Kenya, James Macharia, alikanusha madai kuwa Shirika la Ndege la Kenya, linaendesha ndege zinazosimamiwa na baadhi ya watu wanaopanga kuchukua usukani wa viwanja vya ndege nchini humo.

Wafanyakazi wa Viwanja vya Ndege wanataka usimamizi wa shirika hilo pamoja na Mamlaka ya Kusimamia Viwanja vya Ndege ubadilishwe.

"Hali ilivyo sasa ni kwamba, kuna wasafiri ambao wanaingia, kwa hiyo lazima tusubiri wasafiri wote, kabla ya kuondoka na hatutaondoka kabla ya wasafiri wote kufika, lakini natarajia kuwa mwisho wa siku mambo yatakuwa mazuri," alisema Sebastian Mikosz.

Muungano wa wafanyakazi hao, umehoji ni vipi Shirika la Ndege la Kenya litachukua usimamizi wa mamlaka hiyo ilhali limekuwa likipata hasara ya mabilioni ya fedha kila mara.

Pia umesema hatua hiyo itachangia hasara ya mabilioni ya fedha pamoja na wafanyakazi wengi watapoteza ajira.

Kwa kipindi cha miezi 18 iliyopita, Katibu Mkuu Mtendaji wa Shirika la Ndege la Kenya, Sebastian Mikosz, Mwenyekiti wa Bodi wa shirika hilo, Michael Joseph na wakurugenzi kadhaa walilipwa dola milioni 13, hali iliyotiliwa shaka na muungano wa wafanyakazi.

Wafanyakazi hao pia wanataka wasimamizi hao watimuliwe kutokana na ubadhirifu wa fedha. **DW**




Mamia ya wanafunzi wakiwa wamekusanyika katikati ya Jiji la Algiers, tayari kuandamana kumpinga Rais Abdelaziz Bouteflika kuwania awamu ya tano ya urais. **PICHA: AP**

# Maandamano yapamba moto Algeria

**ALGIERS,** Algeria

MAANDAMANO ya kuipinga serikali yameendelea Algeria wakati Rais wa nchi hiyo, Abdelazizi Bouteflika, akitarajia kutangaza rasmi kugombea muhula wake wa tano.

Rais Bouteflika (82) aliyedumu madarakani tangu mwaka 1999 alielekea Uswisi jana jioni, kwa kile kilichoelezwa anakwenda kufanyiwa vipimo vya kawaida kujua hali yake ya kiafya.

Maandamano katika barabara za miji mbalimbali ya Algeria yalianza siku 10 zilizopita wakati Rais Bouteflika alipotangaza nia yake ya kugombania tena nafasi ya urais.

Maandamano hayo kwa sehemu kubwa yamefanyika katika hali ya amani tofauti na yaliyofanyika mwishoni mwa wiki ambayo yalikuwa makubwa, ambapo mtu mmoja alifariki dunia na wengine 40 kujeruhiwa.

Rais Bouteflika kwa muda mrefu hajaonekana hadharani na amekuwa akitumia kiti cha mgonjwa tangu alipopatwa na kiharusi mwaka 2013. **VOA**

## Waasi wa ADF wawaachia huru mateka

**KINSHASA,** Congo

WAASI wa kundi la ADF la nchini Uganda, wanaoendesha harakati katika misitu ya wilaya ya Beni, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), wamewaachia huru mateka 22.

Mateka waliochukuliwa kutoka vijiji mbalimbali vya Wilaya ya Beni walikuwa wakitumiwa na wapiganaji wa ADF kusafirisha bidhaa walizopora na kulima mashamba yao.

Wakazi wa mji huo walijawa na furaha, ya kuwaona ndugu zao waliotekwa nyara na ADF wakiwa hai.

Waasi wa ADF wamekuwa na tabia ya kuwaua mateka baada ya kuwatumia kama wachukuzi, au kuwaorodhesha katika kundi lao na kuwafanya kuwa wapiganaji.

Kuachiwa huru kwa mateka hao sio jambo la kawaida kwa kuwa wengi wameshapoteza maisha katika misitu wanamoishi waasi wa Uganda ADF katika wilaya ya Beni, na wengine kusajiliwa katika kundi hilo la uasi.

Akizungumza na wanahabari katika mji mdogo wa Eringeti walikowasili mateka hao baada ya kusindikizwa na wapiganaji wa kundi hilo hadi eneo la Mayisafi, mashariki mwa Eringeti, Mjumbe maalumu wa Gavana wa Mkoa wa Kivu ya Kaskazini Eringeri, Njiamoja Sabiti, aliwahimiza wanajeshi wa Kongo kuwavamia na kuwaua waasi hao. **DW**

## Mgogoro Uganda, Rwanda wazidi kutokota

**KAMPALA,** Uganda

SERIKALI ya Uganda kupitia Waziri wake wa Mambo ya Nje, Richard Sezibera, imeishtumu Rwanda kwa kuzua habari za uongo kwamba inawapa hifadhi waasi wa kundi la RNC linaloongozwa na Jenerali Kayumba Nyamwasa kwa lengo la kuhatarisha usalama wa Rwanda.

Imesema kuwa haina lengo lolote la kuchochea vurugu au kuhatarisha usalama wa nchi yoyote jirani.

Mvutano wa kidiplomasia kati ya nchi hizo umeendelea kushuhudiwa baada ya Rwanda kudai kuwa Uganda inawapa hifadhi maadui wa serikali yake, huku Uganda ikikanusha kuhusika.

Vilevile, serikali ya Uganda imekanusha madai yaliyotolewa na Rwanda kuwa inawatesa raia wake. Wizara ya Mambo ya Nje jijini Kampala, imesema madai hayo ya Rwanda hayana msingi na ni ya uongo.

Mvutano kati ya nchi hizo ulizuka baada ya Rwanda kufunga mpaka wake na Uganda katika eneo la Katuna. Hata hivyo, Kigali imekanusha kufunga mpaka huo na Uganda lakini pia kutuma wanajeshi wake mipakani.

Hivi karibuni, Waziri Sezibera alinukuliwa akisema raia wa nchi yake wanateswa nchini Uganda, madai ambayo serikali ya Uganda iliyakanusha. **RFI**

HABARI KITAIFA

# Katoliki watoa waraka mzito

INATOKA UK. 2

familia, yanakuwa ni jambo binafsi na la faragha bila kuhusisha jamii na wala kumhusisha Mungu," TEC inaeleza zaidi katika ujumbe wake huo.

TEC inaeleza kuwa kila mwaka hutoa ujumbe mahsusi katika kipindi cha Kwaresima na huwa na dhamira maalum ya kuzingatia.

"Ili katika kujitafakari na kuamsha upya maisha yetu ya imani Katoliki na maadili yake, tutambue zaidi na tukiri kwa dhati jinsi hali yetu ilivyo mbele ya Mungu ambaye ndiye chanzo cha utakatifu," TEC inaeleza katika ujumbe wake huo.

"Sisi kama wadhambi tulio safarini kuelekea huo utakatifu, kwa mwaka huu wa 2019 baada ya kuadhimisha miaka 150 ya Kanisa Katoliki Tanzania mwaka jana, tumeona ujumbe wa mwaka huu uzingatie dhamira inayohusu familia zetu.

"Dhamira hii ya familia kama kanisa la nyumbani na shule ya imani na maadili, kwa mwaka huu basi, tutafakari kwa namna gani hili lifanyike kwa kuzingatia kuwa familia ya kikristu ni shule ya imani Katoliki na maadili yake."

TEC imeainisha kuwa hoja ya kuitafakari familia mwaka huu imetokana na dhana potofu na hata nadharia zisizo sahihi zinazolenga kuhalalisha vitendo vinavyosababisha kutenganishwa kwa ndoa na familia.

"Kutenganisha huku kunatokana na dhana yenye maana potofu ya ndoa inayotolewa kwamba ndoa ni maridhiano ya wawili bila kufungamanishwa na jinsia zao," TEC inaeleza katika ujumbe wake huo na kufafanua zaidi:

"Hii ni maana potofu inayotetewa na baadhi ya jamii. Hii ni dhana iliyopotoka kihulka, kiimani na kimaadili. Imani ya Katoliki na maadili yake inapingana kabisa na mtazamo wa namna hii, au hoja zinazoweza kutokana na mtazamo kama huo."



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Posta Tanzania (TPC), Hassan Mwang'ombe (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu mkakati wa shirika hilo kuimarisha maduka yake ya kubadilishia fedha za kigeni nchini, ikiwa ni siku chache baada ya taarifa kutoka Benki Kuu. Kushoto ni Meneja Mkuu Uendeshaji Biashara, Mwanaisha Said na Meneja Mkuu Rasilimali za Shirika, Macrice Mbodo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Malalamiko yamkera bosi MOI

**Na Mary Geofrey**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI), Dk. Respocious Boniface, amewataka watumishi wa hospitali hiyo kutoa taarifa ya kila jambo linaloendelea kwa wagonjwa na ndugu wanaofika kupata huduma kwao ili kupunguza malalamiko.

Vilevile, amewataka watoa huduma wa hospitali hiyo kujiepusha na vitendo vya rushwa kwa kuwa si tu imekatazwa kisheria, bali pia ni dhambi.

Dk. Boniface alitoa agizo hilo jana alipozungumza na watumishi wanawake wa taasisi hiyo wakati wakitoa msaada kwa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi wanaopatiwa matibabu katika hospitali hiyo.

Misaada iliyotolewa ina thamani ya Sh. milioni nne na msaada huo ni sehemu ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani ambayo huadhimishwa Machi 8.

Alisema taasisi hiyo imesifiwa na Rais John Magufuli kuwa inafanya kazi zake kwa weledi, lakini kuna changamoto ya watoa huduma kutorudisha taarifa kwa wagonjwa au ndugu zao juu ya kile kinachoendelea.

"Taasisi ya MOI tunajitahidi kutoa huduma kwa weledi na malalamiko yamepungua kwa kiasi kikubwa na Rais Magufuli ametoa pongezi kwa kazi nzuri tunazofanya," Dk. Boniface alieleza na kuongeza:

"Isipokuwa jambo moja tu, tuzingatie kutoa taarifa kwa wagonjwa wetu, kuwa nini kinaendelea wanapokuwa kwenye foleni au wakipatiwa matibabu, ndugu nao waelezwe nini kinaendelea, mfano ndugu yao yupo chumba cha upasuaji muda mrefu, anapaswa kuambiwa kile kinachoendelea badala ya kumwacha tu akiwa na wasiwasi."

Aliwataka watumishi hao kujiepusha na vitendo vya rushwa ambavyo ni chukizo mbele ya jamii huku akisisitiza kuwa hafurahishwi kuona watumishi wake wakitiwa hatiani kwa kashfa hiyo.

Katibu wa Wanawake wa MOI, Caroline Soleko, alisema walichanga fedha kupitia umoja waa huo kwa ajili ya kununua vifaa vya kutoa misaada kwa wagonjwa wao. Alisema wametoa msaada kwa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi wa MOI na wagonjwa wa saratani walioko Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

## Serikali yatahadharisha

INATOKA UK. 2

athari hasa kwa waishio maeneo hatarishi kama mabondeni," alisema.

Alisema Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), ilishatahadharisha kuwa mvua zinazotarajia kunyesha mwaka huu zitakuwa kubwa.

"Napenda kuwasisitizia wananchi wachukue tahadhari, walio mabondeni na wanaoishi kwenye nyumba zilizotitia wahame mapema kabla ya mafuriko," alisema Makonda.

Alisema ujenzi holela na tabia ya watu kutupa taka kwenye mifereji na mito ndiyo imekuwa chanzo kikubwa cha mafuriko na kuwataka wananchi kuacha tabia hiyo.

Katika hatua nyingine, Makonda aliwataka Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (Tarura), kuziba viraka katika barabara ambazo zimekuwa zikisababisha usumbufu na kero kwa watumiaji wa miundombinu hiyo.

"Natoa siku saba Tarura kuziba viraka walivyochimba barabarani kuepusha madhara hasa katika kipindi hiki ambacho mvua zimeanza kunyesha," alisema.

Makonda alisema haiwezekani Tarura wachimbe mashimo halafu yakae miezi miwili bila kufanyiwa marekebisho yaliyokusudiwa. Aliwaagiza Wakala wa Barabara nchini (Tanroads), kusafisha miundombinu ikiwamo mito, mitaro na madaraja yaliyoziba hali ambayo alisema inaweza kusaidia kupunguza athari za mafuriko.

## Mwalimu aanguka kizimbani

INATOKA UK. 2

namba 2,3,4,5,6 na 8 walitoa ushahidi unaoendana na kesi iliyowasilishwa mahakamani.

Alisema kuwa kwa mujibu wa madaktrari wawili kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera, Felix Otieno na Daktari Bingwa wa Magonjwa na Vifo kutoka Hospitali ya Rufani Bugando ya jijini Mwanza, Dk. Kaima Kackson, kifo cha mwanafunzi huyo kilitokana na kupigwa sehemu mbalimbali za mwili.

Alisema ushahidi uliotolewa na madaktari hao waliopata fursa ya kuchunguza mwili wa marehemu, unaonyesha mwanafunzi alikufa kwa kupigwa katika maeneo mbalimbali ya mwili, ushahidi ambao uliendana na uliotolewa na wanafunzi ambao walifika mahakamani kutoa ushahidi na kudai kuwa Mwalimu Respikius alimpiga mwanafunzi huyo kwa fimbo isiyokuwa ya kawaida.

Baada ya kutolewa kwa adhabu hiyo dhidi yake, Mwalimu Mtazingira alianguka kizimbani na kushindwa kuinuka. Askari polisi na magereza waliokuwa karibu na kizimba hicho, walimwinua mwalimu huyo na kumsaidia kutoka kwenye kizimba hicho.

Jaji Mlacha, baada ya kutoa adhabu hiyo, aliwataka walimu na watu wote kupitia kanuni na sheria za elimu ili kufanya kazi yao kwa weledi kama sheria zinavyowataka.

Jaji huyo alisema mshtakiwa alitumia saa tatu kumwadhibu mwanafunzi huyo huku akizunguka naye maeneo mbalimbali ya shule hiyo.

Awali, Wakili wa Serikali, Hashimu Ngole, alidai kuwa Upande wa Jamhuri ulijiridhisha kuwa mwalimu huyo alimpiga na kumsababishia kifo mwanafunzi huyo, huku akidai kuwa hawakulenga kupata ushahidi wa kupotea kwa pochi, bali kujua aliyempiga mwanafunzi hadi kufa.

Alidai hakuna shahidi hata mmoja aliyemtaja Mwalimu Harieth kumpiga mwanafunzi tofauti, isipokuwa pochi ya mwalimu huyo ilipotea na ndiyo ikawa sababu za mwanafunzi huyo kupigwa.

Wakili wa Utetezi wa mshtakiwa wa pili, Aaron Kabunga, aliishukuru Mahakama kwa kutenda haki na kuendesha kesi hiyo haraka.

Alidai kesi hiyo ilikuwa na nguvu katika jamii kwa kuwa jamii ilitamani haki itendeke haraka juu ya tukio hilo la mauaji na ndiyo sababu ya watu wengi kufurika mahakamani jana kusikiliza hukumu yake.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MASHAMBA/VIWANJA

**KIWANJA KINAUZWA,** Kiwanja kilichopo Bagamoyo Mkoa wa Pwani,eneo la Sanzale "B" lenye Sq.meters 3920 linauzwa. Eneo hilo limepimwa na lina hati ya umiliki. Linafaa kwa shughuli za kibiashara, kujenga kituo cha kuuzia mafuta nk. Kwa maelezo zaidi piga simu Na.0715 263 683/0784 263 683.

**ENEO LINAUZWA,** NAUZA ENEO LIKO MPIJI MAGOE YANAPOGEUKIA MAGARI YA KUTOKA MBEZI NI UNATEMBEA MITA 200 HADI KWENYE ENEO UKUBWA NI MITA 20@40. BEI NI NAFUU KABISA SIMU NAMBA: 0621 607825.

### MAGARI/VIPULI

**LEYLAND DAF ZINAUZWA,** DAF TANKI YA MAJI LITA 10,000, DIESEL CC 5880. DAF PICK UP DIESEL CC 4200 TANI 4.5. MAGARI YAPO KWENYE HALI NZURI ZOTE ZINATEMBEA. MAWASILIANO: 0657 370655 DAR ES SALAAM.

### MCHANGANYIKO

**PATA RAMANI ZA MAJENGO MBAL**imbali kama vile ramani za nyumba,shule na kadhalika.Mawasiliano;0744113969

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.

### CHETI KIMEPOTEA




**MWANAIDI MGAYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0468-0040** kilichotolewa na shule ya sekondari KIRIKI mwaka 2009.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**MAG/PS/A.24/39/A/VOL.**

115098202

### KUPOTEA KWA CHETI



**Mafuru Godfrey** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S2530/0085** kilichotolewa na Baraza la Taifa mwaka 2014 katika shule ya Sekondari Nyamanoro, Mwanza . Na pia anatangaza kupotelewa na Result Slip vyote vilipotelea mkoani Mwanza Kilimahewa.

Yeyote atakaeviona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**NY/RB/800/2018**

115097802

### CHETI KIMEPOTEA



**NEEMA MGHAMBA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0654-0062** kilichotolewa na shule ya sekondari Rwambaizi mwaka 2009.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KGD/RB/4726/2019.**

115097902

### KUFUNGA KWA KAMPUNI

Wamiliki wa Kampuni ya **EASTERN AFRICA FAIR TRADE NETWORK** yenye namba ya usajili **68793** wanapenda kuwataarifu Umma kuwa Kampuni yao imemaliza shughuli zake na hivyo kuifunga Kampuni hii kwa mujibu wa Sheria za Makampuni Sura ya 212 mapitio ya 2002. Imetolewa na Wakurugenzi wa Kampuni leo tarehe 06.03.2019.

115100002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**J/PCF.54**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA ( MCA/63)**

**Mahakama ya mwanzo ya MAKOLE**

**wilaya ya DODOMA**

**MADAI NAMBARI 10 YA 2019**

**MDAI.............................RAHMAT JANUARY Anamdai**

**MDAIWA.............................SHEILANI BASHIRU JUMA**

**Kwa SHEILANI BASHIRU JUMA**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**

**MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unahitajiwa /mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya Tarehe 13/3/2019 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikidhibitisha kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshundwa /mmeshindwa kutekeleza kwa amri yangu na chapa ya mahakamahii leo tarehe 4/3/2019

215099602

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JOSHUA MUROWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 321 CFL BMW.** Chassis namba **WBAFA52010LM56389.** Engine namba **306S565654343.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KMR/RB/2512/2019.**

115099402

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HINDI AARON TORROHA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 402 CEL VOLKSWAGEN.** Chassis namba **WVWZZZ9CZYM616779.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KMR/RB/2512/2019.**

115099302

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Kishen Enterprises Ltd** anatangaza kupotea kwa kadi yenye usajili wa namba T228 CQE aina ya BAJAJ-TOYO, yenye chasis namba KEFKE600003705, engine namba 163FML2D1476092.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**WMB/RB/2200/2019**

115098802

### KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**ABDALLAH HEMED** anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI aina TOYOTA COASTER yenye namba za usajili **T 527 APJ.** Chassis **BB210018543,** Engine Namba **3B123802.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOM/TR/RB/2649/2018.**

115099502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: **MJINI MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No; 57/2019**
Ombi la **FRIDA MWANSASU** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **YOYO ANTHONY NAKAME**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/04/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 05/03/2019.

215097202

### KUFUNGA KWA KAMPUNI

Wamiliki wa Kampuni ya **AFRICA FAIR TRADE NETWORK** yenye namba ya usajili **55642** wanapenda kuwataarifu Umma kuwa Kampuni yao imemaliza shughuli zake na hivyo kuifunga Kampuni hii kwa mujibu wa Sheria za Makampuni Sura ya 212 mapitio ya 2002. Imetolewa na Wakurugenzi wa Kampuni leo tarehe 06.03.2019.

215099902

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO, NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# PIRES AMPELEKA ZIDANE CHELSEA

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane, ametajwa kuwa chaguo bora zaidi la kuinoa klabu ya Chelsea na kuchukua nafasi ya Maurizio Sarri.

Mchezaji mwenzake nguli kwenye timu ya Taifa ya Ufaransa, aliyewahi kung'ara na Klabu ya Arsenal, Robert Pires, amemtaja akimpa sifa kuwa ndiye 'shujaa atakayeineemesha Chelsea'.

"Nadhani Zidane anaweza kuwa chaguo bora zaidi kwa Chelsea. Anaweza kupata heshima kutoka kwa wachezaji wa Chelsea na kudhibiti nidhamu kwenye chumba cha kubadilishia nguo kama matokeo ya kazi nzuri aliyoifanya uwanjani na kama kocha," Pires aliwaambia waandishi wa habari.

"Alikuwa mshindi na mpiganaji. Ana mafanikio mazuri kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kitu ambacho kinamvutia mmiliki wa Chelsea. Itakuwa habari njema kwa Ligi Kuu kama Zidane ataenda England," aliongeza.

Hata hivyo, Pires ameushushia lawama uongozi wa Klabu ya Chelsea kwa namna wanavyoishi na makocha wa klabu hiyo, akimwelezea Sarri kuwa ni kiongozi mzuri na mwenye historia nzuri ya mafanikio, lakini wameshindwa kumtunza vema.

Katika hatua nyingine, Pires alidai kuwa anamuona Kylian Mbappe kama mshindi wa Ballon d'Or katika siku za usoni.

"Ni nyota mkubwa na mchezaji mzuri sana, anaweza kufikia viwango vya Cristiano Ronaldo na Lionel Messi. Ni muda tu ukifika atashinda Ballon d'Or," alisema.

Alisema Mbappe anafanya vizuri katika ligi ya aina yoyote na ameanza kupewa heshima kubwa uwanjani akiwa na umri wa miaka 20 tu.




# United wajipanga kumsajili Dybala

**MACHESTER,** England

KLABU ya Manchester United itaangalia uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Juventus, Paulo Dybala, wakati wa kipindi hiki cha majira ya joto kama Romelu Lukaku ataondoka.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji anaonekana kuwa kwenye rada za kuwaniwa na klabu ya Juventus msimu huu, baada ya kupoteza namba kwa Marcus Rashford, ingawa amefunga mabao manne katika mechi zake mbili zilizopita.

Na kama mchezaji huyo wa zamani wa Everton hataamua kuondoka kipindi cha majira ya joto, Gazeti la The Sun limedai kuwa Manchester United watakuwa wanaangalia uwezekano wa kumtafuta mbadala wa Lukaku kwa kumsajili Dybala.

United tayari imeshaulizia dau la kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ambazo ni pauni milioni 120, uhamisho ambao utaweka rekodi klabuni hapo na kuivunja ile iliyowekwa na Paul Pogba ya pauni milioni 94.5.

Dybala awali alikuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia kwenye Ligi Kuu ya England, lakini alikataa kujiunga na Arsenal wakati alipokuwa anaondoka Palermo mwaka 2015, na badala yake akahamia kwa miamba hao wa Turin kwa pauni milioni 36. Amecheza mechi 172 kwa Bianconeri hao tangu alipojiunga nao na kufunga mabao 77 na kutoa pasi za mwisho 31.

Huku Dybala akipewa nafasi ya kutakiwa kumrithi Lukaku hapo Old Trafford, Manchester United kwanza watatakiwa kumuuza kwanza mshambuliaji huyo wakati wa kipindi cha majira ya joto.

# Mourinho hana nafasi Real Madrid – Solari

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Klabu ya Real Madrid, Santiago Solari, ametoa kejeli na vicheko kuhusu tetesi kuwa kocha wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho, anaweza kuchukua kibarua chake hivi karibuni.

Hatua hiyo imekuja ikiwa ni siku mbili tangu Mourinho azungumzie uwezekano wa kukinoa tena kikosi cha Real.

Solari ambaye ameonyesha kuchekelea tetesi hizo, amedai kuwa klabu hiyo imewahi kuwa na waigizaji zaidi ya wale wa Hollywood, akimtaja mrembo Julia Roberts.

"Klabu hii imewahi kuwa na waigizaji wengi zaidi ya Julia Roberts," alisema Salari. Julia ni muigizaji nguli wa kike wa Marekani, maarufu zaidi katika tamthilia za mapenzi.

Uchokozi wa waandishi wa habari kuhusu jina alilolitaja ulienda mbali na kumuuliza ni nani kati yake na Mourinho ambaye Julia angemchagua ili ale naye bata.

"Katika sekta hiyo, ingepaswa kumuuliza yeye [Julia] mwenyewe," alijibu.

Wikendi iliyopita, Mourinho ambaye hivi sasa hana kibarua baada ya kutimuliwa na Manchester United Desemba mwaka jana, aliiambia beIN SPORTS kuwa yuko tayari kurejea Real Madrid katika siku za usoni.



HABARI MICHEZO

# Salah aachwa kikosi Misri

**CAIRO,** Misri

KOCHA wa Misri, Javier Aguirre, hajamjumuisha Mohamed Salah katika kikosi chake cha timu ya Taifa na hivyo amempa nafasi ya kupumzika nyota huyo wa Liverpool.

Salah amekuwa akishutumiwa kwa kuwa kwenye kiwango kibovu katika siku za hivi karibuni kutoka kwa mashabiki, wakati 'Wekundu' hao wakiwa wamezidiwa kete na Manchester City kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu.

Hata hivyo, Liverpool sasa imepata habari njema kwenye mbio za ubingwa huo baada ya kocha wa Misri, Aguirre, kumuacha Salah kwenye mchezo unaofuata, akiamini kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 atapata nafasi nzuri ya kujiimarisha.

Misri inapanga kucheza na Niger kwenye michuano ya kufuzu Afcon Machi 22, mwaka huu, lakini Farao hao tayari wameshajihakikishia nafasi ya kufuzu kucheza michuano hiyo, na hivyo Aguirre ameona hana haja ya kumjumuisha Salah kwenye mchezo ujao.

Pia timu hiyo itaivaa Nigeria siku nne baadaye katika mchezo wa kirafiki, lakini Salah pia atabaki na Liverpool.

Licha ya kufunga mabao 17 katika mechi 29, Salah amefunga bao moja tu katika mechi zake sita za Ligi Kuu, huku kikosi hicho cha Jurgen Klopp kikipitwa pointi moja na Manchester United baada ya kutoka sare na Everton mwishoni mwa wiki.

Na matokeo yake, Liverpool ipo nafasi ya pili na City inaongoza kwa tofauti ya pointi moja.

Liverpool sasa watacheza na Fulham Machi 17, lakini Salah atakuwa na kama wiki mbili za mapumziko kabla ya kwenda kuwavaa Tottenham Hotspur Machi 31, mwaka huu.



# POCHETTINO APIGWA FAINI PAUNI 10,000



**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino, atatumikia adhabu ya kukosa mechi mbili na amelimwa faini ya pauni 10,000 kutokana na utovu wa nidhamu aliofanya dhidi ya mwamuzi, Mike Dean kwenye mchezo dhidi ya Burnley.

Kikosi cha Pochettino kilifungwa mabao 2-1 kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Turf Moor, na raia huyo wa Argentina hakuridhishwa na maamuzi ya Dean.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, Chama cha Soka cha England (FA), kilisema: "Mauricio Pochettino ametozwa faini ya pauni 10,000 na atatumikia adhabu ya kukosa mechi mbili.

"Kocha wa Tottenham Hotspur amekubali adhabu hiyo kwa utovu wa nidhamu aliouonyesha kwenye mchezo dhidi ya Burnley Februari 23, mwaka huu."

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 47, juzi Jumanne aliweza kuiongoza timu yake kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuwatoa miamba wa Bundesliga, Borussia Dortmund kwa jumla ya mabao 4-0.

# *Solari: Matokeo hayanikatishi tamaa*

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Santiago Solari, amesema hana mpango wa kukata tamaa baada ya kipigo cha mabao 4-1 kutoka kwa Ajax kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa na kujikuta wakitolewa kwenye mashindano hayo.

Kutolewa kwa Madrid kwenye mshindano hayo kunamaanisha kwamba, matumaini ya kutwaa taji lolote msimu huu hayapo, kwani wametolewa kwenye Coa de Rey na nafasi nzuri kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga ikiyeyuka.

Ajax waliwafumua Real Madrid kwenye dimba lao la nyumbani la Santiago Bernabeu baada ya kufungwa mabao 2-1 kwenye mchezo wa kwanza wa hatua hiyo ya mtoano wa timu 16-bora.

Sasa presha kwa kocha huyo raia wa Argentina imekuwa kubwa zaidi baada ya kupoteza mechi tatu mfululizo na wamepitwa pointi 12 na vinara wa La Liga, Barcelona.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Solari aliwaambia waandishi wa habari: "Sikuja kwenye klabu hii ili nikate tamaa wakati mambo yanapokuwa magumu.

"Kitu tunachotakiwa kufanya ni kubakia kuwa watulivu katika wakati huu mgumu.

"Madrid ni timu kubwa kuliko yeyote kati yetu hapa - mara zote huwa inarudi kwenye uimara wake."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DE JONG: BARCA CHANZO KUITOA R. MADRID UEFA

●●● Ni ushahidi kwamba kinda huyo ajaye wa Barcelona ameonyesha matarajio ya...

**MADRID,** Hispania

KINDA wa Ajax mwenye kipaji cha hali ya juu dimbani, Frenkie de Jong, amefunguka kuwa klabu yake ijayo, FC Barcelona, ilimtaka kuwatoa wapinzani wao wakubwa, Real Madrid, kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wakifanya mazungumzo ya kujiunga na klabu hiyo.

**Real Madrid imejikuta ikitupwa nje na Ajax kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora kufuatia kuchapwa mabao 4-1 juzi [hivyo kutolewa kwa jumla ya mabao 5-3].**

Kipigo hicho kimekuja ikitoka kuchapwa mechi mbili mfululizo hivi karibuni na Barcelona kwenye Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'] na katika mchezo wa La Liga, na ushindi huo wa Ajax unawafanya 'Los Blancos' hao kupoteza mechi nne mfululizo katika uwanja wao wa nyumbani, Santiago Bernabeu msimu huu.

Lakini De Jong aliyekamilisha uhamisho wake wa kujiunga na Barcelona majira ya baridi na akitarajiwa kutua Catalunya majira haya ya joto, ametoa siri ya juhudi zake hadi kuitoa Real Madrid.

Akijulikana kwa ukomavu na maono yake akiwa na mpira, kinda huyo wa Kiholanzi mwenye umri wa miaka 21, alionyesha uwezo wake dhidi ya Real Madrid juzi usiku na kudhihirisha thamani yake ya euro milioni 75.

Dhidi ya wapinzani kama Luka Modric na Toni Kroos, aliutawala uwanja na kuwatawala viungo wa Real Madrid. Na sasa Mholanzi huyo amefunguka kuwa Barcelona ilimtaka kuitoa Real Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya kukutana Santiago Bernabeu juzi.

"Nilizungumza nao wakati nilipotsaini mkataba na waliniambia nijaribu kuitoa Real Madrid, na kwamba hilo litakuwa jambo jema kwa Barca pia," De Jong aliliambia Gazeti la Uholanzi, De Telegraaf, kama alivyonukuliwa na ESPN.

Sasa ni ushahidi kwamba kinda huyo ajaye wa Barcelona ameonyesha matarajio ya kubeba majukumu makubwa kufuatia kuwatoa Los Blancos hao.

Kinadharia kipigo hiki kinahitimisha msimu wa tabu wa Los Blancos, kwa kuwa itaumaliza bila kombe lolote, kwani sasa inahitaji muujiza tu kuweza kutwaa La Liga.

Real Madrid tayari imetolewa kwenye Kombe la Mfalme na Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati huu ikiwa imekaa katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa La Liga, pointi 12 nyuma ya vinara wa ligi hiyo, Barcelona.

Ajax sasa inarejea Ligi Kuu Uholanzi ambapo itaivaa Fortuna Sittard na kisha Zwolle, wakati Real Madrid ikiwa na kibarua kigumu kwenye La Liga dhidi ya Real Valladolid kabla ya kuwavaa Celta Vigo.

## ZISIKUPITE

### DYBALA MBADALA WA LUKAKU

MANCHESTER United inaandaa pauni milioni 120 ili kutoa ofa ya kumnasa mshambuliaji wa Juventus na Argentina, Paulo Dybala 25, kama Romelu Lukaku, 25, ataondoka Old Trafford majira haya ya joto. ***(Sun)***

### OVERMARS KUHAMA NA DE LIGT

MKURUGENZI wa Soka wa Ajax, Marc Overmars, amesema angependa kumsajili beki wa kati wa klabu hiyo, Matthijs de Ligt, 19, kama atajiunga na klabu nyingine. Overmars amekuwa akihusishwa kuchukua nafasi hiyo katika klabu yake ya zamani, Arsenal. ***(Mirror)***

### INIESTA AVUTA SAMPER JAPAN

ANDRES Iniesta anajaribu kumshawishi kiungo Mhispania mwenzake Sergi Samper, 24, kuondoka Barcelona na kujiunga na Vissel Kobe ya Japan. ***(Reuters)***

### MASHABIKI KUCHAGUA KOCHA

MASHABIKI wa Real Madrid, wamepewa nafasi ya kupiga kura endapo kila mchezaji katika kikosi hicho auzwe na kuchagua kocha gani aajiriwe. ***(Marca - in Spanish)***

### DONNARUMMA KUFUNGWA

MAJADILIANO ya mkataba yameanza kati ya Milan na kipa Gianluigi Donnarumma. Milan ipo tayari kumwoongezea mkataba. ***(SportMediaset, via Calciomercato)***

### CHILWELL KUVUNJIWA BENKI

MANCHESTER City itapaswa kuvunja rekodi ya dunia ya uhamisho kwa kutoa pauni milioni 75 ili kumsajili beki, ambazo Liverpool ililipa kwa beki wa kati Mholanzi Virgil van Dijk, 27, kama watataka kumsajili beki wa kushoto wa Leicester City na England, Ben Chilwell, 22. ***(Telegraph)***

### CHELSEA, UNITED ZATUA LILLE

CHELSEA inavutiwa kumwajiri Mkurugenzi wa Michezo wa Klabu ya Lille, Luis Campos, ambaye pia amekuwa akihusishwa na majukumu hayo Manchester United. ***(France Football, via Star)***

### ALLEN AMTABIRIA BALE EPL

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Tottenham, Clive Allen, amesema klabu za London zinaweza kuwa na "kauli nzito" ya kumsajili mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale, 29, kutoka Real Madrid. ***(Talksport)***

### RICE SASA KUICHEZEA ENGLAND

KIUNGO wa West Ham, Declan Rice, 20, anajiandaa kujumuishwa katika kikosi kijacho cha England kitakachoshiriki kuwania kufuzu michuano ya Ulaya ijayo baada ya FA kukamilisha taratibu za kuichezea timu hiyo akitokea Jamhuri ya Ireland. ***(Telegraph)***

### MAGUIRE AMTESA RODGERS

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers, anatambua kuwa atakabiliana na vita kali ya kumbakisha Harry Maguire majira haya ya kiangazi, wakati huu Manchester United ikivutiwa na beki huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 26. ***(Leicester Mercury)***

### BAMBA ATOA NENO CARDIFF

BEKI wa Cardiff City, Sol Bamba, 34, ameitaka klabu yake kuepuka kushuka daraja, licha ya nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast kuwa nje ya dimba kwa kipindi chote kilichobaki msimu huu. ***(Mirror)***

# KMKM yajiimarisha kuchukua ubingwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya KMKM kufanikiwa kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, kocha wa timu hiyo, Ame Msimu, amesema anaamini atanyakuwa ubingwa wa ligi hiyo msimu huu kwa sababu kikosi chake kipo imara na kina uwezo wa kukamilisha malengo hayo waliyojiwekea.

Mabaharia hao wa KMKM wanaongoza ligi hiyo wakiwa na pointi 52 wakati nafasi ya pili inashikiliwa na Malindi yenye pointi 50, huku Maafande wa KVZ ambao walikuwa vinara kwa muda mrefu wao wameshuka hadi nafasi ya tatu wakiwa na pointi 49.

Hata hivyo, KMKM na Malindi wao wamecheza michezo 23 wakati KVZ wana mechi moja pungufu.

Msimu alisema wachezaji wake wameimarika na sasa wanatumia vema nafasi za kufunga wanazopata tofauti na ilivyokuwa katika mzunguko wa kwanza.

Kocha huyo aliongeza kuwa katika soka, lolote linaweza kutokea na kusema kwamba mzunguko wa lala salama ni mzunguko wenye "maajabu" kutokana na kila timu inapambana kuhakikisha inamaliza katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea tena keshokutwa Jumamosi kwa Mafunzo kukutana na Hardrock wakati KVZ wataikaribisha Jamhuri huku New Star wakivaana na Chuoni na Selem View wao watachuana na Polisi kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba.

## MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 26 | 20 | 4 | 2 | 43 | 17 | 64 |
| 2. Azam | 26 | 15 | 8 | 3 | 36 | 17 | 53 |
| 3. Simba | 20 | 16 | 3 | 1 | 43 | 7 | 51 |
| 4. Kinondoni MC | 28 | 9 | 14 | 5 | 31 | 18 | 41 |
| 5. Lipuli | 29 | 9 | 11 | 9 | 24 | 26 | 38 |
| 6. JKT Tanzania | 29 | 8 | 12 | 9 | 17 | 18 | 36 |
| 7. Alliance | 29 | 9 | 9 | 11 | 23 | 30 | 36 |
| 8. Mbao | 28 | 9 | 9 | 10 | 19 | 26 | 36 |
| 9. Mtibwa Sugar | 26 | 10 | 5 | 11 | 26 | 21 | 35 |
| 10. Mbeya City | 27 | 9 | 7 | 11 | 27 | 29 | 34 |
| 11. Coastal Union | 28 | 7 | 13 | 8 | 26 | 30 | 34 |
| 12. Ruvu Shooting | 29 | 8 | 10 | 11 | 27 | 35 | 34 |
| 13. Kagera Sugar | 27 | 7 | 12 | 8 | 21 | 25 | 33 |
| 14. Mwadui | 29 | 9 | 6 | 14 | 31 | 36 | 33 |
| 15.Stand Utd | 29 | 9 | 6 | 14 | 27 | 37 | 33 |
| 16. Ndanda | 27 | 8 | 9 | 10 | 17 | 27 | 33 |
| 17. TZ Prisons | 28 | 7 | 11 | 10 | 20 | 24 | 32 |
| 18. Singida Utd | 27 | 8 | 8 | 11 | 20 | 26 | 32 |
| 19. Biashara Utd | 27 | 5 | 9 | 13 | 18 | 29 | 24 |
| 20. African Lyon | 29 | 4 | 10 | 15 | 18 | 36 | 22 |

# AZAM FC YATANGAZA KUHAMIA NYAMAGANA

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya serikali kutangaza kuufunga Uwanja wa Taifa na Azam Complex, vyote vya jijini Dar es Salaam ili kukamilisha maandalizi kuelekea Fainali za Vijana za Afrika (AFCON U-17), uongozi wa Azam FC umetangaza kuhamia kwenye Uwanja wa Nyamagana ulioko Mwanza.

**Uwanja wa Nyamagana unamilikiwa na Jiji la Mwanza na una nyasi bandia kama ulivyo Uwanja wa Azam Complex, ulioko Chamazi jijini.**

Akizungumza jana jijini, Meneja wa Azam FC, Philipo Alando, alisema klabu yao imeamua kutumia Uwanja wa Nyamagana katika mechi zake za nyumbani wakati ambao uwanja wao wa Azam Complex utakuwa kwenye matayarisho ya kutumika katika fainali za AFCON U-17.

Alando ambaye timu yake imepangwa kukutana na Kagera Sugar katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA, alisema tayari klabu yao imeshakamilisha taratibu za maombi ya kutumia uwanja huo na wanaamini uamuzi wao ni sahihi.

"Mwezi huu tutacheza na Kagera Sugar mara mbili, mechi ya Ligi Kuu na mechi ya Kombe la FA, ni mechi ambazo zitakuwa ngumu maana tutakutana ndani ya muda mfupi, yote kwa yote tumejipanga kuhakikisha tunachukua ubingwa wa michuano hii mwaka huu," alisema Alando jana, baada ya kumalizika kwa droo ya hatua ya robo fainali.

Alisema wanahitaji kushinda kombe hilo na kukamilisha historia ya klabu yao kwa kushinda mataji yote kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati.

"Tunajiandaa kuhakikisha tunachukua ubingwa wa Kombe la FA, hii ndio kiu yetu sasa, tuchukue ubingwa na tupate nafasi tukaiwakilishe nchi katika mashindano ya kimataifa. Pia tukichukua ubingwa kabati letu litakuwa limeenea na historia itakuwa imeandikwa," aliongeza Alando.

Naye Meneja wa Kagera Sugar, Mohammed Hussein, alisema mechi hiyo ya robo fainali itakuwa ngumu na wao kama wenyeji watapambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na kusonga mbele katika michuano hiyo.

Ubingwa wa mashindano hayo uko wazi baada ya aliyekuwa bingwa mtetezi, Mtibwa Sugar kuiaga michuano hiyo baada ya kukubali kufungwa na KMC ya jijini Dar es Salaam.



Omar Kunambi (kulia) wa timu ya DTB akiwazuia washambuliaji wa timu ya Buyuni FC katika mechi ya mwisho ya sitabora Kanda ya Dar es Salaam iliyochezwa juzi. Mechi hiyo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Singida United, Popadic kumalizana*

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Singida United umesema utakaa meza moja na benchi la ufundi la timu hiyo linaloongozwa na Mserbia, Dragan Popadic ili aweze kuendelea kufundisha timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Popadic ameipa klabu hiyo siku tisa ili kumaliza changamoto ya mishahara yake na upatikanaji wa huduma zinazostahili kwa wachezaji wake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa timu hiyo, Festo Sanga, alisema wanatarajia kukutana na Popadic ili kumaliza changamoto hiyo kwa sababu bado wanahitaji huduma ya makocha hao.

Sanga alisema mbali na tatizo la mishahara, kuhusu chakula ambacho kocha huyo alikilalamikia alisema kuwa ni mlo wa ndizi na nyama ambao ni wa kawaida kwa Watanzania.

"Tutayamaliza kabla ya hizo siku tisa walizotoa, suala la chakula kuleta mkanganyiko kwetu halikuwa tatizo, timu ilipikiwa ndizi na nyama, hiki ni chakula cha kawaida tulichokizoea," Sanga alifafanua.

Aliongeza kuwa mpaka sasa mazungumzo yao yamefikia katika hatua nzuri, na wanaamini hawatavunja mikataba ya makocha hao kwa sababu wanahitaji kufanya vizuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya Kombe la FA.

# Michezo



Alhamisi Machi 7, 2019

Nipashe

## De Jong: Barca chanzo kuitoa Real Uefa

HABARI UK. 30




David Neres akimzidi ujanja kipa Thibaut Courtois na kuifungia Ajax bao la pili wakati ikishinda 4-1 na kuitoa Real Madrid kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa jumla ya mabao 5-3. Mechi hiyo ya marudiano ilipigwa Uwanja wa Santiago Bernabeu juzi. **HABARI UK. 29**

# Kagere, Bocco watoa neno kwa JS Saoura

## Morali waongezeka Algeria, Simba ikirudi mechi zake Ligi Kuu kuhamishia Morogoro huku...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI wachezaji wa Simba wakisema wanaamini watapata matokeo chanya katika mechi dhidi ya JS Saoura itakayochezwa keshokutwa, Jumamosi nchini Algeria, uongozi wa klabu hiyo umeuchagua Uwanja wa Jamhuri, Morogoro kuwa uwanja wake wa nyumbani katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya ule wa Taifa kufungwa kwa muda kwa maandalizi ya Afcon U-17.

**Mechi hiyo kati ya JS Saoura dhidi ya Simba itachezwa kuanzia saa 4:00 usiku wakati mchezo mwingine wa Kundi D utaanza saa 1:00 usiku ukiikutanisha AS Vita dhidi ya Al Ahly itakayochezwa mjini Kinshasa, Jamhuri ya Kidemkorasia ya Congo.**

Nahodha wa Simba, John Bocco amesema kuwa wamekwenda Algeria kwa kazi moja ya kusaka ushindi ingawa wanafahamu haitakuwa kazi rahisi.

"Tumejiandaa na kujipanga kwa ajili ya kutafuta ushindi, tunajua pia wenzetu wamejiandaa na mechi hii, tunajua faida ya nyumbani, lakini kwa upande wetu tunasema mpira kokote," alisema mshambuliaji huyo.

Naye mshambuliaji Mnyarwanda, Meddie Kagere, aliliambia gazeti hili kuwa uwezo na nia ya kushinda mchezo huo wanao na sasa kilichobakia ni kuhakikisha wanatimiza mipango yao.

"Tukiwa tumebadili akili zetu kuelekea katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tunaamini tunaweza kupata ushindi na kutinga hatua ya robo fainali na nusu fainali, kwa umoja na ushirikiano tulionao na mashabiki, hakuna kisichowezekana," Kagere alisema.

Wakati huo huo, mashabiki wa Simba jana waliendelea kujitokeza kusaidia maandalizi ya Uwanja wa Jamhuri ambao watautumia katika mechi zao za ligi zinazofuata.

Mwakilishi wa Simba mkoani humo, Shabani Nyaa aliliambia gazeti hili kuwa wamefurahi kupata heshima hiyo na wanaahidi watatoa ushirikiano kwa uongozi ili kufanikisha kushinda mechi zote zitakazochezwa kwenye uwanja huo.

"Baada ya kumaliza mechi zao za Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba itakuwa mwenyeji dhidi ya Ruvu Shooting hapo Machi 19, mwaka huu, tunaendelea na maboresho ya uwanja na kabla ya siku hiyo, tunaamini kila kitu kitakuwa vema, wadau na watu mbalimbali wamejitokeza kusaidia matengenezo, ushirikiano huu maana yake tuko tayari," alisema Nyaa.

Simba ipo nafasi ya pili katika msimamo wa Kundi D ikiwa na pointi sita, moja nyuma ya vinara Al Ahly ikifuatiwa na JS Saoura yenye alama tano huku AS Vita ikiburuza mkia kwa pointi nne.

# Yanga, Azam hadi fainali FA

**Na Somoe Ng'itu**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga na mabingwa wa Kombe la Kagame, Azam FC zote za jijini Dar es Salaam, uwezekano wa kukutana kwenye Kombe la FA mwaka huu, unaweza kutokea tu endapo timu hizo mbili zitafanya vema kwenye mechi zao za hatua ya robo fainali na nusu fainali ya michuano hiyo na kisha kukutana fainali, na si vinginevyo, imefahamika.

Mshindi wa mashindano hayo atapata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika hapo mwakani.

Yanga ambayo imepangwa kucheza ugenini na Alliance FC katika mechi ya hatua ya robo fainali, endapo itaibuka mshindi katika mchezo huo, itakutana na mshindi wa robo fainali nyingine kati ya Lipuli FC ya Iringa na Singida United ya mkoani Singida.

Kwa mujibu wa droo ambayo ilichezeshwa jana, pia inaonyesha kuwa mshindi kati ya mechi nyingine ya robo fainali itakayowakutanisha Kagera Sugar dhidi ya Azam FC, atacheza mchezo wa hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo dhidi ya mshindi kati ya KMC FC dhidi ya African Lyon, zote za jijini.

Yanga ilifanikiwa kutinga hatua ya robo fainali kwa kuwafunga Namungo FC ya Lindi bao 1-0 wakati Azam FC wenyewe waliwaondoa Rhino Rangers ya Tabora kwa kuwapa kichapo cha mabao 3-0.

Ratiba ya mashindano hayo yanayosimamiwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), inaonyesha kuwa mechi hizo za hatua ya robo fainali ya michuano hiyo itachezwa kati ya Machi 28-31, mwaka huu.

Akizungumza kuhusu droo hiyo, Msemaji wa Yanga, Dismas Ten alisema watajipanga vizuri zaidi kwenda kuwakabili Alliance FC kwa sababu wanafahamu Mwanza ni "pagumu".

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >